SportPesa
TZS. 735,865,580
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Korti** yakataa kupokea nyaraka za komandoo

UKURASA 4



**Guardiola: Kiwango City hakijashuka misimu sita**

UKURASA 22

Jumanne Novemba 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580780

www.ippmedia.com
...com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Shahidi: Wasaidizi wa Sabaya walidai ni maofisa wa TISS

• **Pia** walimtisha ni wa TRA, hivyo asingewapa fedha...*Ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**MUHIMBILI YAPANDIKIZA ULOTO KUTIBU SARATANI**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imevunja rekodi nyingine kwa kuwapandikiza uloto (bone marrow transplant)...

**Wadaiwa sugu NHC kuondolewa mwezi ujao**

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni wakishika mfano wa funguo ikiwa ni ishara ya uzinduzi rasmi wa Shule ya Awali na Msingi ya Museveni iliyojengwa kwa msaada wa Rais huyo wa Uganda wilayani Chato mkoani Geita, jana. **PICHA: IKULU**



Mkurugenzi wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (watatu kushoto), akipokea Tuzo ya Huduma Bora za Fedha kwa njia ya kidijitali Afrika Mashariki kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Diplomasia ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Edwin Rutegaruka, jijini Dar es Salaam, Juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Museveni atoboa siri ujenzi shule 3 nchini

UKURASA 3

**MICHEZO** **MORRISON AOMBA RADHI SIMBA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Askari wa Suma JKT pamoja na Mgambo wa Jiji wakifanya usafi katika stendi ya zamani ya Mwenge na kuondoa meza zote zilizowekwa na wafanyabiashara wadogo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUDY MNZAVA**

# Wadaiwa sugu wa NHC kuondolewa mwezi ujao

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) linatarajia kuanza kuwaondoa wapangaji wa nyumba zake ambao ni wadaiwa sugu kuanzia mapema mwezi ujao.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, wakati akizungumza na wapangaji wa shirika hilo jijini Mwanza ukiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kikazi kukagua utekelezaji wa shughuli za sekta ya ardhi na NHC pamoja na kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi changamoto za ardhi.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, NHC inadai takriban Sh. bilioni 26 kwa wapangaji wa nyumba zake jambo alilolieleza linachangia kuzorotesha kasi ya utendaji kazi wa shughuli za kila siku za shirika ukiwamo ukarabati.

"Tutachofanya sasa, yeyote aliyelimbikiza deni na tushampa notisi, lakini bado halipi kodi basi zoezi la kumwondoa litafanyika bila hata kumtaarifu upya," alisema Dk. Mabula.

Aliongeza kuwa, operesheni ya kuwaondoa wadaiwa sugu wa nyumba za NHC itaenda sambamba na kuwaondoa wapangaji wote wasio waaminifu waliopangisha nyumba za shirika kwa gharama nafuu, huku nao wakipangisha watu wengine kwa gharama kubwa ambapo alikielezea kitendo hicho ni kuiibia serikali na halikubaliki kwa kuwa ni kosa kisheria.

Aliwahakikishia wapangaji wa nyumba za NHC kuwa, shirika hilo limeanza kufanya ukarabati wa nyumba zake ikiwa ni mpango wake wa miaka mitano na tayari kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 50 kimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliliomba shirika hilo kuona namna ya kuzifanyia marekebisho baadhi ya nyumba zake hasa upakaji upya wa rangi baada ya serikali kuwapanga upya wafanyabiashara wadogo maarufu kama wamachinga maeneo ya miji ili kupendezesha mji.

Naye Meneja wa NHC Mkoa wa Mwanza, Fadhili Anyegile, alisema, kwa mwaka wa 2021/2022 shirika hilo limeweka mikakati ya kuhakikisha linapunguza malimbikizo ya madeni ya wapangaji kwa asilimia 100 kutoa elimu kwa wapangaji juu ya utaratibu wa kulipa kodi kwa wakati na kuendelea na zoezi la kufanya matengenezo makubwa na madogo katika nyumba zake ili kuzifanya kuendelea kuwa imara.

# Shahidi: Wasaidizi wa Sabaya walidai ni maofisa wa TISS

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFANYABIASHARA Francis Mroso (44), amedai alitoa Sh. milioni 90 ili kuokoa maisha yake kwa kuwa vijana waliokuwa wameambatana na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, walijitambulisha kuwa ni maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS).

Shahidi huyo pia amedai mahakamani kwamba baadhi ya vijana hao walijitambulisha ni maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) na wanahusika na ukusanyaji wa kodi.

Vilevile, shahidi huyo amedai kwamba Sabaya na vijana wake, walimtishia kwamba wangempoteza endapo angeshindwa kutoa kiasi hicho cha fedha.

Shahidi huyo wa 10 katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda, wakati akiendelea kutoa ushahidi wake.

Shahidi huyo alidai Sabaya alimwambia asipotoa fedha hizo, watampoteza, hivyo aliingiwa na hofu ya kupotezwa na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi ambayo haina dhamana.


Katika kesi hiyo, mbali na Sabaya washtakiwa wengine, katika shauri hilo ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, shahidi huyo alidai kwamba kampuni yake ya Mrosso Injector Pump Services imeanza kufanya kazi mwaka 2015.

Shahidi huyo alidai biashara yake imesajiliwa na kuendeshwa kwa kufuata kanuni, sheria na taratibu zote za nchi.

Shahidi huyo alidai kwamba ni utaratibu wake kutoa risiti za kielektroniki wakati anapomaliza kutoa huduma katika biashara hiyo.

Alidai kuwa katika biashara yake hiyo, hajawahi hata siku moja kukwepa kulipa kodi ya serikali wala hajawahi kutoa rushwa.



Alidai katika uendeshaji wa biashara yake, aliwahi kutoa rushwa kwa kulazimishwa kutoa fedha na Sabaya.

"Hapana mimi siyo mtoa rushwa kwa kuwa sikutoa kwa hiari yangu kwa kuwa nililazimishwa kutoa rushwa," alidai shahidi.

Akizungumza mahakamani huko, shahidi huyo alidai kwamba alitishiwa kwamba asipotoa fedha hizo atafunguliwa kesi ya uhujumu uchumi na atapotezwa.

"Vijana wa Sabaya waliniambia kwamba Sabaya, amepewa wadhifa wa kuwa kiongozi wa kikosi kazi maalumu cha kuwakamata watu wanaouhujumu uchumi kwa kanda ya kaskazini na kuwafungulia kesi na kazi ya kushughulika na wakwepaji wa kodi, aliteuliwa kutekeleza jukumu hilo na aliyekuwa Rais Hayati Dk. John Magufuli," alidai.

Shahidi huyo alidai kwamba alitoa fedha hizo kwa kuwa aliyemtishia maisha ni kiongozi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na ni mteule wa Rais, hivyo alipata hofu.

Alidai kwamba akiwa na watu hao ambao walijitambulisha kuwa maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa, alitoa fedha ili kuokoa maisha yake kwa kutokupotezwa.

"Sikuweza kutoa taarifa polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kuwa nilizuiwa kuzungumza na simu kwa wakati huo," alidai shahidi huyo.

Mroso alidai mahakamani huko kwamba akiwa katika Benki ya CRDB Tawi la Kwa Murombo jijini Arusha, alishindwa kumweleza meneja na watoaji wa huduma wa benki kwa kuwa alikuwa chini ya ulinzi wa vijana wa Sabaya.

"Nilishindwa kupiga kelele kuomba msaada kuwa natishiwa maisha na kulazimishwa kutoa hela kwa kuwa vijana wale walijitambulisha kwangu ni maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa, hivyo nilishindwa kufanya chochote, nilidhani watakuwa ni askari," alidai shahidi huyo.

Alidai kwamba vijana waliokuwa wameambatana naye hadi benki, mmoja ndio alimtambua kwa jina la Watson Mwahomange lakini wengine hakuwatambua kwa majina bali kwa mwonekano wao.

"Wakati tukielekea nyumbani kwangu, Sabaya aliniambia nitoe kiwango hicho cha fedha, vinginevyo wangeondoka na mimi," alidai shahidi huyo.

Alidai kuwa akiwa benki, aliulizwa na mhasibu wa benki hiyo kwamba anatoa kiasi hicho cha fedha alithibitisha kwamba ni kweli kwa kuwa kuna mtu anataka kumlipa.

"Siyo wajibu wa maofisa wa benki hiyo kufahamu, kuuliza, kutaka na kujua kwamba fedha ninatoa benki kwa kazi gani," alidai shahidi.

HABARI KITAIFA

# Museveni atoboa siri ujenzi shule 3 nchini

**Na Richard Makore,** CHATO

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametumia sehemu kubwa ya hotuba yake kusimulia mahusiano yake na Tanzania, huku akitoa siri iliyomfanya ajenge shule tatu za msingi nchini.

Kadhalika, ametoa siri kwamba asilimia 68 ya wananchi wake ni watu wa kufanyia 'tumbo na mfuko' yaani wanalima kwa ajili ya kupata fedha kidogo ya kuweka mfukoni, lakini hawaangalii namna ya kupiga hatua kimaendeleo.

Akihutubia mamia ya wananchi na viongozi mbalimbali wilayani Chato mkoani Geita jana, wakati akikabidhi shule ya msingi iliyopewa jina lake, Museveni alieleza historia yake na Tanzania ikiwamo kilichomsukuma kurudisha shukrani.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, wakati wa vita ya Tanzania na Uganda chini ya utawala Iddi Amini, (Museveni) aliishi katika kijiji cha Nyamiaga kilichopo mpakani mwa Tanzania na Uganda, katika nyumba ya nyasi na kwamba baada ya kufanikiwa kuchukua nchi na kuwa Rais wa Uganda, alimuomba Hayati Benjamin Mkapa atoe msaada kwa kujenga shule eneo hilo.

Alisema katika kipindi chote cha mapigano ya kumuondoa Amini aliishi hapo na kwamba aliamua kujenga shule hiyo, ili iwe zawadi kwa wanakijiji hicho lakini pia kama kumbukumbu.

Aidha, alisema shule nyingine ameijenga katika kijiji cha Muhutwe wilayani Muleba,ambayo alieleza kuwa ilitokana na kuishi katika nyumba moja ya mzee Zakaria Masoud mwaka 1978, wakati wa vita ya Uganda.

Alisema alipokuja Tanzania katika ziara yake pia alimuomba hayati Mkapa ajenge shule katika kijiji hicho cha Muhutwe na hivyo kuitwa Shule ya Msingi Muhutwe.

"Nilipokuja ziara nilienda kumuona Mzee Zakaria Masoud na nikamkuta na familia yake, niliamua kutoa zawadi kwa wananchi wa kijiji hicho kwa kuwajengea Shule ya Msingi," alisema Museveni.

Alisema shule ya tatu aliamua kuijenga Chato baada ya hayati Dk. John Magufuli kumkubalia afanye hivyo na kwamba yeye alikubaliana naye, ingawa alisisitiza kwamba hakumuomba kufanya ujenzi huo.

"Hii ni mara ya kwanza kitu kama hiki kuitwa jina langu na hata duniani hakuna kitu cha kijamii kinaitwa jina langu, hata kule kwangu Uganda sitaki kuitwa jina langu vitu vya kijamii,"alibainisha Rais Museveni.

Aliongeza kuwa kitu pekee kilichomfanya kujenga shule hizo ni undugu alionao na Tanzania pamoja na kuweka kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kuhusu wananchi wake kuwa wavivu kwenye kilimo licha ya kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba, Rais Museveni alisema hatua hiyo inawakwamisha kufikia maendeleo.

Kwa mujibu wa Rais Museveni, Waganda wengi wanalima kwa ajili ya tumbo, kwa maana ya kupata chakula pamoja na kupata fedha kidogo za kuweka mfukoni.

Aliongeza kuwa kati ya kaya 2,500 moja pekee ndiyo inayofunga walau nguruwe kwa ajili ya kuongeza kipato, lakini waliobaki hawajishughulishi na kazi nyingine.

"Kwa namna hii nchi haiwezi kupiga hatua za maendeleo kwa watu kufanyia tumbo na mfuko na kushindwa kufanya kazi nyingine," alibainisha.

### SAMIA AMSHUKURU

Kwa upande wake, Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza katika makabidhiano hayo ya shule hiyo, alimshukuru Rais Museveni kwa kuwekeza kwenye elimu.

Alisema shule hiyo itakayokuwa na mitaala ya Kiingereza yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 630, imegharimu dola za Marekani milioni 1.6.

Rais Samia alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na Uganda katika nyanja mbalimbali za kiuchumi ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maendeleo.

Akizungumzia suala la wanafunzi wa shule za sekondari kuruhusiwa kuendelea na masomo wanapopata ujauzito, alisema suala hilo lisichukue muda mwingi kujadiliwa kwa kuwa limeishapitishwa na serikali.

Alisema mwanafunzi wa shule ya msingi akipata ujauzito hataendelea na masomo katika mfumo wa kawaida badala yake atafundishwa njia nyingine ya ujasiriamali na kujiajiri, lakini wale wa sekondari wao wataruhusiwa kuendelea na masomo.

Alisisitiza kuwa wanafunzi wote walioacha shule kutokana na utoro na mimba warudi shule na kuendelea na masomo na wale walioshindwa mitihani ya darasa la saba wapewe nafasi ya kurudia shule.

Akizungumza katika sherehe hizo za makabidhiano, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema serikali imeongeza bajeti ya elimu bure kutoka Sh. bilioni 21 kwa mwezi hadi kufikia Sh. bilioni 26 kwa mwezi.

Aidha, aliagiza kila kiongozi kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa fedha za Uviko-19 unakamilika kabla ya Desemba 15, mwaka huu, ili kuwezesha wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza kuanza masomo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekonolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema wanafunzi 9 07, 802 waliomaliza darasa la saba mwaka huu wamepangiwa kuendelea na masomo ya sekondari.

Alisisitiza kwamba wanafunzi walioacha masomo warudi shuleni na serikali itawapa nafasi nyingine ili kurudia masomo na wakifaulu wataendelea kusoma katika mfumo rasmi wa serikali.


**UBALOZI WA SWITZERAND, SWISS COOPERATION AGENCY(HPSS), INTRAHEALTH INTERNATIONAL NA HTT INFRACO TANZANIA.**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Switzerland, Swiss Cooperation Agency (HPSS), Intrahealth International na HTT Infraco Tanzania Limited, watauza kwa mnada wa hadhara Magari tarehe 4 December, 2021Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Magari yatakayouzwa:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Toyota Land Cruiser Hard Top | 1HZ Diesel Engine | 2013 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser GX | 1HZ Diesel Engine | 2011 | Haujalipwa |
| 4 | Nissan Patrol S/Wagon | ZD 30Diesel Engine | 2016, | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Patrol S/Wagon | VK56 Petrol Engine | 2013 | Umelipwa |
| 1 | Ford Everest Station Wagon | P5A Diesel Engine | 2016 | Haujalipwa |
| 1 | Tata Pick Up 3.5 ton 709 Turbo | Diesel Engine | 2011 | Umelipwa |

**Magari yote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 30 Nov. mpaka 3 December, 2021, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.**

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 10 December,2021 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.**
3. Magari yote yatauzwa kama yalivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Magari yote yaliouzwa yatatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu **atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.**
7. **Kila mtu anayesiriki mnada ni lazima kuvaa Barakoa na kunawa na maji tiririka auSanitaiza, Umbali wa mtu na mtu uzingatiwe. Kwa maelezo zaidi waone:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
Cell Number- +2550754 284926 E-mail:universalauction@hotmail.com
Insta:universalauctioncentre Dar es salaam

116592502


# Muhimbili yapandikiza uloto

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imevunja rekodi nyingine kwa kuwapandikiza uloto (bone marrow transplant) wagonjwa watano wa saratani mbalimbali za damu.

Aidha, inajipanga kuanza huduma ya upandikizaji mimba (IVF) nayo inatarajiwa kuanza kutolewa hospitalini hapo Februari mwakani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Lawrence Museru, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio makubwa yaliyofikiwa na hospitali hiyo.

Alisema utolewaji wa huduma ya upandikizaji wa uloto, umeifanya Tanzania iandike historia nyingine kwenye utoaji huduma bobezi katika nchi zilizopo ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Hatua hii ni kuunga mkono jitihada za serikali kuanzisha huduma ambazo zilikuwa hazipatikani kutokana na kutokuwapo wataalamu pamoja na miundombinu stahiki ya kutolea huduma hizi kwani mgonjwa wa aina hii akienda nje ya nchi hugharimu Sh. milioni 250, kwa kuanzisha huduma hii nchini itagharimu Sh. milioni 70.

"Na katika kutimiza hili, serikali mwaka jana ilitoa kiasi cha Sh. bilioni saba ili kuwezesha uanzishwaji wa huduma hizi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kituo cha umahiri katika upandikizaji, sehemu ya fedha hizi zimewezesha kununua vifaa na kusomesha wataalamu na hatimaye tumefanikiwa kuanzisha huduma za upandikizaji uloto."

Prof. Museru alisema kwa kuanzia, wanategemea kupandikiza angalau wagonjwa 48 kwa mwaka sawa na wagonjwa wanne kila mwezi kwa sababu watalaamu na miundombinu stahiki ipo.

"Huduma hii ya upandikizaji tunayoitoa ina kiwango sawa na mgonjwa anayepandikizwa sehemu yeyote duniani. Huduma hii inatolewa kupitia hospitali zetu mbili ambapo hapa Upanga ni shughuli za uchunguzi na kule Mloganzila ni upandikizaji kutokana mgonjwa huyo kuhitaji mazingira maalumu. Mazingira ya Mloganzila yanaruhusu huduma hiyo kufanyika na kutunzwa kwa viwango stahiki," alibainisha.

Alisema utolewaji wa huduma hiyo unaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kupandikiza uloto katika Ukanda wa Afrika Mashariki na pia nchi ya sita katika Bara la Afrika ambazo ni Afrika ya Kusini, Tunisia, Misri, Morocco, na Nigeria. "Takribani wagonjwa 200 wanahitaji huduma ya upandikizaji kwa mwaka," alisema.




Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, akiwasilisha taarifa ya mafanikio na mwelekeo wa wizara hiyo kwa waandishi wa habari jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## KESI YA MBOWE

# Korti yakataa kupokea nyaraka za komandoo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imekataa kupokea nyaraka za upande wa utetezi kama kielelezo, ikisema shahidi amekuwa mchumi wa maneno na ameshindwa kueleza wakati ambao kielelezo hicho alikutana nacho.

Uamuzi huo wa mahakama wa kukubali pingamizi la upande wa Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, ulitolewa jana mbele ya Jaji Joackim Tiganga baada ya kuzingatia hoja za pande zote mbili.

"Ni wazi wakili lazima akutane na shahidi wake wakati wa kumwandaa kabla ya kutoa ushahidi, lakini kwa bahati mbaya sana, maelezo haya yametolewa na wakili sio shahidi, shahidi hakusema alipata nafasi ya kuonana na wakili.

"Shahidi amekuwa mchumi sana wa maneno, ameshindwa kueleza mahakama alikutana na kielelezo wakati gani na kuonyesha ana uelewa na kielelezo," alisema Jaji.

Akisoma uamuzi huo alisema mahakama imeridhika kwamba mshtakiwa ambaye ni shahidi wa utetezi kwenye kesi ndogo, Mohammed Ling'wenya, ametaja vitu vilivyomo kwenye barua ambavyo ni sahihi ya wakili, jina lake na muhuri wa mahakama hivyo akitupilia mbali hoja ya kwanza ya Jamhuri kupinga barua hiyo.

Katika ushahidi wake wiki iliyopita, Ling'wenya alidai ni komandoo.

Jaji huyo alisema ni vigumu kukuta barua ina vitu vitatu kwa maana hiyo Mahakama imeona shahidi ameweza kueleza vilivyopo kwenye kielelezo.

"Sasa mahakama inahamia kwenye mnyororo wa kielelezo, eneo hili mahakama imeelezwa kwamba mtiririko haukuthibitika na upande wa mashtaka umeeleza kwamba ili uweze kutoa nyaraka ya mshtakiwa lazima barua iwe imehusisha magereza.

"Wanasema isipokuwa tu shahidi anapokuwa kwenye kizimba, akiwa mahakakamani wakili anaruhusiwa kuwasiliana na shahidi kwa maana hiyo wakili lazima akutane na shahidi wake wakati wa kumwandaa kabla ya kutoa ushahidi.

"Lakini kwa bahati mbaya sana maelezo haya yametolewa na wakili sio shahidi, shahidi hakusema ni wakati gani alipata nafasi ya kuonana na wakili.

"Shahidi amekuwa mchumi sana wa maneno, ameshindwa kueleza mahakama alikutana na kielelezo wakati gani na kuonyesha ana uelewa na kielelezo, shahidi kuona pekee ushahidi haitoshi kuonyesha kwamba alikuwa na umiliki wa kielelezo hicho," alisema Jaji Tiganga.

Alisema shahidi hakueleza alifanyia nini barua hiyo, hivyo mahakama inashindwa kuamini kwamba alikiona kielelezo hicho.

Alisema barua aliyotakiwa kutoa mahakamani ni ile aliyopeleka kwa RPC Ilala na hiyo aliyotaka kutoa sio nakala yake, ni barua iliyogongwa muhuri na Naibu Msajili sio RPC Ilala.

"Kwa namna hiyo shahidi ameshindwa kuonyesha mtiririko kwa sababu kashindwa kueleza ilikuaje kielelezo alishindwa kukitoa akatoa barua iliyogongwa muhuli na Naibu Msajili, kwa sababu hizo mahakama inakataa kupokea kielelezo hicho," alisema na kuamuru shahidi Ling'wenya kuendelea kutoa ushahidi wa upande wa utetezi katika kesi ndogo ndani ya kesi kubwa ya ugaidi.

Wakili wa utetezi Dickson Matata, alimwongoza shahidi huyo ambaye alidai hajawahi kufika Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam ndio maana aliandika barua kwa RPC Ilala kuomba taarifa kama Agosti 7 mpaka 9 mwaka 2020 alikuwa kituoni huko.

Akihojiwa na Wakili Nashon Nkungu, alidai tangu akamatwe Moshi Agosti 5 hadi anafikishwa mahakamani Agosti 19 mwaka 2020, zilikuwa zimefika siku 14.

Akihojiwa na Wakili John Mallya, shahidi huyo, alidai aliyemwokoa kwenye mateso Moshi ni mtu mmoja aliyeamuru askari waache kumpiga lakini hamfahamu mtu huyo.

"Ni uongo kwamba tulipokamatwa tulizunguka kumtafuta Moses Lijenje, mimi sijawahi kutoka mahabusu tangu nifikishwe Kituo cha Moshi.

"Sikupata huduma ya chakula, vitendo walivyokuwa wananifanyia niliona mateso, Mahita alinipiga na rungu kwenye nyayo, Koplo Goodluck kwenye gari alikuwa ananitisha, aliniambia watanitupa huku akinichoma choma na kitu kama bastola kwenye mbavu.

"Tazara nilipofikishwa sikuandikishwa popote, barua niliyoandika kwa RPC Ilala nilitaka kujua pia Koplo Msemwa alikuwa Kituo cha Polisi cha Kati Agosti 7 mwaka 2020, lakini nilichoomba sijapata mpaka leo (jana)," alidai.

Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala, shahidi huyo alidai hakuwahi kumwona Mkuu wa Kituo kuthibitisha Koplo Msemwa alikuwa kituoni siku hiyo, mahabusu na askari wenzake aliowahi kufanya nao kazi hawakuwa na sababu ya kumdanganya kuhusu kuwapo Kituo cha Polisi Tazara.

Ling'wenya alidai hakuna askari aliyewahi kumpa simu ili awasiliane na ndugu zake na upande wa utetezi ulimaliza kumhoji mshtakiwa huyo wa tatu anayedai aliteswa, alitishwa kusainishwa karatasi na hakuwahi kufikishwa Kituo cha Polisi cha Kati kama inavyodaiwa alifikishwa na kuchukuliwa maelezo.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, shahidi alidai katika ushahidi wake hajatoa taarifa ya kitabibu kuonyesha alipigwa na alipofikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Agosti 19, mwaka 2020.

Alidai alimwambia Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba kuhusu mateso wakati maelezo ya mashahidi yanasomwa.

"Mateso hata gerezani nilikuwa naendelea kuyapata, tangu nikamatwe nilikuwa najisaidia nikiwa na pingu," alidai.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Ling'wenya na Halfani Bwire ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama Kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020 kufanya vitendo vya kigaidi.

# Dawa uvamizi maeneo ya JWTZ yapatikana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Stergomena Tax, amesema wizara yake imepanga kupima maeneo yote ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kuyapatia hatimiliki, ili kukomesha migogoro ya ardhi inayosababishwa na wananchi kuyavamia.

Dk. Stergomena alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara yake kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema jeshi hilo hadi sasa tayari limeshapima maeneo 56 na mengine 96 yapo katika mpango wa kupimwa, ili yaweze kupata hatimiliki.

"Tumepanga kupima maeneo yote yenye migogoro tayari 56 tumeshayapima bado mengine 96, ambayo yapo katika mpango wa kupimwa katika maeneo mbalimbali Tanzania bara,"alisema Dk. Stergomena.

Alisema JWTZ inahitaji ardhi kwa ajili ya ujenzi wa makambi, makazi ya wanajeshi na maghala ya kuhifadhia silaha.

Vilevile, waziri huo alisema jeshi hilo linahitaji ardhi kwa ajili ya kuendeshea mafunzo na mazoezi mbalimbali ya kijeshi.

"Kutokana na maeneo mengi ya jeshi kutokupimwa kuliwapa wananchi fursa ya kuyavamia. Hali hii inataokana na utaratibu uliokuwapo kwamba maeneo yote ya serikali ikiwamo Jeshi la Ulinzi la Wanachi wa Tanzania (JWTZ) hayakupimwa na kupatiwa hatimiliki,"alisisitiza.

Alisema mwongozo wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wa mwa 2016, unaruhusu Taasisi za umma ikiwamo jeshi kumiliki ardhi kwa hatimiliki.

"Kazi ya upimaji, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yanayomilikiwa na jeshi imeanza na itakuwa endelevu, ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya jeshi unaofanywa na wananchi,"alisema

Kadhalika, alisema kazi hiyo inafanyika kupitia mpango wa miaka mitatu yaani 2020/21 hadi 2022/2023.

Aidha, alisema katika kutekeleza mpango mkakati huo wizara imefanikiwa kupima jumla ya maeneo 56 kazi iliyofanyika katika awamu mbili kwa maeneo 17 yaliyopo mikoa ya Tanzania bara.

"Wizara ipo katika kutekeleza awamu ya tatu ya mkakati huo katika mikoa mingine ya Tanzania bara na visiwani yanayofikia 96,"alifafanua.

Pia, alisema baadhi ya maeneo yaliyopimwa, wizara imefanikiwa kupata ramani zilizosajiliwa 38, katika mikoa mbalimbali ya Tanzania bara na ulipaji wa fidia unafanyika kwa kuzingatia uwapo wa uwezo wa kibajeti.

Hata hivyo, alisema wizara hiyo itaendelea kuhakikisha kuwa mipaka ya nchi inaendelea kuwa salama.

## HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (watatu kushoto), akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya jana. Kulia ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga na kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Pancras Bujulo. Habari Uk.7 **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Msajili aitaka CUF kujibu malalamiko ya waliotimuliwa

**Na Sabato Kasika**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeuandikia barua uongozi wa Chama cha Wananchi (CUF), ikiutaka kujibu malalamiko yaliyofikishwa kwenye ofisi hiyo na wanachama wanaodai kuvuliwa uongozi na kufukuzwa katika chama.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisthy Nyahoza, aliliambia gazeti hili jana kuwa ofisi yake inasubiri majibu kutoka katika uongozi wa chama hicho ili iweze kutoa uamuzi wa malalamiko hayo.

"Tuliwapelekea barua hiyo Novemva 26 mwaka huu na wanatakiwa kufikia Ijumaa ya wiki hii wawe wameijibu, ili hatua nyingine za kushughulikia malalalamiko hayo ziendelee kuchukuliwa," alisema Nyahoza.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Magdalena Sakaya, alithibitisha kupokelewa kwa barua hiyo, na kwamba itafanyiwa kazi baada ya kuangalia kile ambacho Ofisi ya Msajili inataka kujibiwa.

"Sipo ofisini, lakini nimepata taarifa za kuwapo kwa barua hiyo, lakini sijajua ni nini kinatakiwa kujibiwa, hivyo viongozi wa CUF tutawasiliana ili kuangalia ni nani wanatakiwa kujibu na nini kinatakiwa kujibiwa," alisema Sakaya.

Alifafanua kuwa inawezekana ni barua inayotakiwa kujibiwa na kiongozi, mmoja au baraza, na kwamba watakapoisoma ndipo watajua imeelekezwa kwa nani, ili ijibiwe haraka iwezekanavyo.

Hivi karibuni, baadhi ya wanachama wa CUF waliwasilisha malalamiko yao katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, jijini Dodoma, wakipinga kuondolewa katika chama hicho wakidai kuwa taratibu hazikufuatwa.

Miongoni mwao ni aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Habari, Uenezi, Uhusiano na Umma wa CUF, Abdul Kambaya wakiwamo pia Ahmed Hamis, Mohamed Vuai, Ali Makame na Mtumwa Ambari.

Wengine waliofukuzwa na Baraza Kuu la CUF chini ya Mwenyekiti wa chama hicho, Prof. Ibrahim Lipumba ni Ahmed Hamis, Mohamed Vuai, Ali Makame, Mtumwa Ambari, Hamida Huweshi na Dhifaa Mohamed Bakari.

Aidha, wanachama hao ambao inaelezwa kuwa walikuwa ni wajumbe wa baraza hilo pia yumo Chande Jidawi aliyekuwa Kaimu Katibu wa Jumuiya ya Vijana wa chama hicho.

# Maeneo yaliyoathiriwa ukame kutembelewa

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Mifugo imesema inajipanga kutembelea maeneo yote yaliyoathiriwa na ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi na kusababisha mifugo kufa na mingine kudhoofu na kulishwa ikiwa imelala.

Juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alisema ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi umesababisha baadhi ya mikoa, ng'ombe na mbuzi kufa.

Kutokana na taarifa hiyo, Nipashe jana ilimtafuta Mkurugenzi wa Idara ya Uendelezaji wa Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, Dk. Asimwe Rwiguza, ambaye alisema taarifa za mifugo kufa na mingine kudhoofu kutokana na ukame walizipata kupitia kwa maofisa mifugo waliopo chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

"Tulifanya tathmini kwa kuwaomba maofisa wa mifugo chini ya TAMISEMI watupatie takwimu halisi, lakini walituleleza ipo mifugo imeanza kufa ila vifo kamili hawakutupa," alisema.

Dk. Rwiguza alisema wanajipanga kufanya ziara kwenda maeneo husika kujua ni mifugo mingapi imekufa kwa tatizo hilo kisha taarifa kamili watazitoa.

"Tumeambiwa mikoa yote ya Pwani na Morogoro ndiyo yenye athari kubwa hususani maeneo ya Ngerengere na Mkata, taarifa tulizopata mifugo imedhoofu wengi wanalishwa wakiwa chini wamelala," alibainisha.

# Vituo 310 vyatangazwa kutumika uchaguzi Ngorongoro

**Na Thobias Mwanakatwe**, NGORONGORO

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetenga vituo 310 kwa ajili ya zoezi la kupiga kura katika uchaguzi mdogo Jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha.

Msimamizi Mkuu wa uchaguzi katika jimbo hilo, Dk.Juma Mhina, akizungumza na gazeti hili jana alisema katika uchaguzi huo watu 115,858 wamejiandikisha kwa ajili ya kupiga kura.

Dk. Mhina ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Ngorongoro, alisema mwenendo wa kampeni kwa wagombea 11 walioteuliwa kuwania ubunge katika jimbo hilo ni mzuri na hakuna malalamiko yeyote hadi sasa.

" Mwenendo wa kampeni ni mzuri, vyama vyote vinazingatia taratibu na kanuni za uchaguzi na vinazingatia ratiba na muda wa mikutano na kuzindua kampeni zao kulingana na ratiba iliyopo na kila chama kimepewa kitabu cha maelekezo ya uchaguzi," alisema.

Dk. Mhina alisema tangu kampeni zimeanza Novemba 16, mwaka huu, wagombea wa vyama vyote wanafanya kampeni kama kawaida na hakuna chama ambacho mgombea wake amekwama kufanya kampeni kutokana na sababu zozote zile.

Aliwataka wagombea na vyama vyao wanapoona kuna jambo halijakaa sawa wasisite kufika katika ofisi za NEC ambazo zipo wazi muda wote na kwamba wasikimbilie kutoa malalamiko kwenye vyombo vya habari. Wagombea na vyama vyao ambao wanachuana katika kinyang'anyiro hicho ni Emmanuel Lekishoni Shanghai (CCM), Simon Jonhson Bayo (SAU), Amina Amiri Mcheka (NLD), Mary Moses Daudi (UPDP) na Frida Marko Nnko wa chama Cha (UMD).

Wengine ni Paulo Mwita Makuru (UDP), Shafii Kitundu (ADC), Feruziy Feruziyson (NRA), Simon P Ngilisho (Demokrasia Makini ), Jonson Gagu (ACT-Wazalendo ) na Zuberi Hamis (ADA TADEA).


## JOB OPPORTUNITY

Tumaini SACCOS is a member based financial institution registered under COOPERATIVE SOCIETY ACT, with the Main objective of giving loans to members in accordance to Loan Policy.

**POSITION: SACCOS MANAGER**
Tumaini SACCOS is based in Arusha, is seeking to recruit suitably qualified candidate for the vacant positions of SACCOS MANAGER

**REPORTS TO: SACCOS CHAIRPERSON**

**GENERAL RESPONSIBILITIES:**
Responsible in exploring potentials that will contribute to SACCO's sustainability, growth, and proper utilization of resources for maximum output

**Duties and Responsibilities**

1. Ensure organization climate where resources are identified, deployed, and exploited efficiently and effectively, through coordination of efforts and resources including Personnel, Capital, and information
2. Ensure attainment of SACCOS Vision, Mission, Policies, and Strategies that will facilitate attainment of SACCOS objectives
3. Supervise and direct resources to portfolio growth
4. Oversee, analyze, interpret monthly, quarterly, and annual reports
5. Advise the Board on Investment decisions
6. To prepare and serve as Board Secretary, responsible in preparing, and keeping Board minutes on timely basis
7. To network with other stakeholders in issues relating to innovations, capacity building, legal, and Technology adoption
8. Champion in all matters relating to Product innovations, and marketing of existing and new product
9. In collaboration with Board chair, undertake all human resource issues including staff motivation, create discipline atmosphere to SACCO staff and capacity building to staff and members
10. Resource person in Policy, and bylaw amendments
11. Oversee all compliance issues and ensure that are done timely
12. Represent Tumaini SACCOS to external forums/networking
13. Carry out any other duties as may be assigned by the Board of Directors

**Required knowledge, Skills and Abilities**
A holder of Master's Degree in Business administration, Cooperative Management, Microfinance, from recognized institution

- Chartered Public Accounting (CPA) will be an added advantage
- Mature Christian person committed to Christian values; including integrity and honesty.
- Ability to work with only occasional supervision.
- Ability to learn new things
- Proved Leadership and management skills
- Negotiation skills
- Training skills
- Creative ability
- Experience with personal computers using Microsoft Office including Excel and Word. Skills working with Loan trucking Software is an added advantage

**Experience**

- Minimum 4 years' experience in SACCOS Management

Employment will be granted upon successful completion of all applicable checks, including last working history and Christian maturity. Only successful applications will be contacted regarding to attend scheduled interviews. If you do not receive any feedback on your application, please consider yourself unsuccessful.

All interested Candidates are required to send application letters, with CV to:

**CHAIR PERSON:**
**TUMAINI SACCOS,**
**BOX 6070, ARUSHA.**
**Email: johnson_robinson@wvi.org**

**Applications should be received not letter than 23 December 2021, official hours.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# W/biashara wachangamkie fursa za biashara nchi jirani

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan alieleza kuwa vikwazo vilivyokuwapo baina ya Tanzania, Kenya na Uganda vilivyodhorotesha biashara vimeondoka, hivyo sasa ni wakati wa wafanyabiashara kuchangamkia fursa, ili kuimarisha uchumi wao na nchi zao.

Alieleza kuwa kutokana na vikwazo hivyo, biashara baina ya nchi hizo ilikuwa ngumu kiasi cha kufikia bidhaa kutoruhusiwa kuvuka mpaka, huku vifaranga kutoka Kenya vikichomwa moto na sukari kutoka Uganda kutoruhusiwa kuingia nchini.

Hali hiyo ilisababisha kila upande kuweka zuio dhidi ya mwingine kwa kuwa viongozi wa maeneo ya mpakani kuwa na uadui ambao uliathiri nchi zote kwa kuwa biashara nyingi zilizuiwa kuingai nchi husika.

Rais alisema kwa sasa vikwazo vyote vimemalizika baada ya kuwapo mazungumzo ya pande zote na sasa ni wakati wa kila upande kuchangamkia biashara ili kudumisha ushirikiano na kunufaisha nchi kiuchumi na kutoa ajira za moja kwa moja na za muda mfupi.

Tunatambua nchi hizi ni Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambao wamekubaliana kupunguza vikwazo vya kibiashara kiasi cha kuondoa baadhi ya masharti kwenye mipaka ili kurahisisha biashara baina ya nchi wanachama wa jumuiya. Kupitia umoja huo nchi hizo zilifikia mahali pa kujadili uwezekano wa kuwa na pasi moja ya kusafiria, umiliki wa ardhi, kuondoa vikwazo vya biashara katika kuelekea katika shirikisho na kuongozwa kuwa na kiongozi mmoja.

Panapojitokeza tofauti ambazo zinasababisha kutokuelewana ni muhimu zikashughulikiwa mapema kabla ya kusababisha madhara makubwa kwa wananchi kama ilivyojitokeza hadi nchi kuwekeana vikwazo kwamba bidhaa za upande huu hazitapita na za huku hazitapita.

Hili linakumbusha jinsi Kenya ilivyotangaza kuwa mahindi kutoka Tanzania yana sumu kuvu, hivyo hayaruhusiwi kuingia nchini humo, kiasi cha magari mengi kukwama kwenye mipaka ya Namanga, Sirasi, Tarakea, Holili na Horohoro.

Baada ya mazungumzo ya viongozi wa pande zote, hali ilirejea na haikuelezwa tena kwamba mazao hayo yameacha kuwa na sumu iliyokuwa inatwaja, jambo linalodhihirisha kuwa kulikuwa na mvutano unaoendelea ambao ulitingisha uhusiano wa nchi husika. Tunatarajia kuona kuimarika kwa biashara baina ya nchi husika kwa kuwa vikwazo vimeondolewa, na wakuu wa nchi hizo wameridhia kushirikiana na kufanya biashara zenye manufaa.

Ni wakati muafaka sasa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kuona fursa nyingi zilizoko Uganda kwa kupeleka bidhaa, kufungua kampuni na ofisi mbalimbali nchini humo ambazo zitaendelea kuzitangaza bidhaa zinazozalishwa nchini.

Kuimarika kwa biashara baina ya nchi na nchi kunasaidia kuboresha uhusiano, kuingizia nchi fedha za kigeni, kuongeza wawekezaji na kukuza uchumi kwa kuwa watu watapata ajira za muda mfupi na za kudumu, mzunguko wa fedha utaongezeka na maendeleo ya miundombinu na watu yataongezeka.

Kutokana na mgawanyiko wa kijiografia nchi zinategemea na kwa mambo mengi kwa kuwa raslimali zipo kwenye nchi tofauti na hakuna iliyojitosheleza kwa kila kitu, na ndiyo maana mpaka unapofungwa wananchi wa nchi fulani wanataabika kwa kukosa mahitaji muhimu ikiwamo chakula.


Tunaipongeza serikali kwa kushughulikia kasoro zilizojitokeza na tunaamini imejengwa misingi imara itakayozuia kujirudia tena, sasa ni wakati wa biashara kustawi baina ya nchi na nchi.

Wafanyabiashara wa Tanzania wasibaki nyuma katika kuchangamkia fursa ili isiwe ni wafanyabiashara kutoka nje wanafanya biashara kubwa bali tuone Watanzania wakiwekeza na kuwa na biashara kubwa zenye kuajiri mamia katika nchi hizo.

Pia wachangamkie biashara ya nchi na nchi inayoletwa na fursa mbalimbali, ikiwamo manufaa ya mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga.

Haitarajiwi kuona vyakula vinatolewa nje bali kampuni zinunue bidhaa zinazozalishwa na Watanzania wenyewe na ajira zitakuwa kipaumbele kwa wazawa ambako mradi unatekelezwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Karata hii TAMISEMI kuongeza ari ya kusoma

**WANAFUNZI** 907,802 wamechaguliwa kuingia kidato cha kwanza Januari, 2022, kwa wakati mmoja baada ya serikali kukamilisha maandalizi ya kuwapokea katika shule walizopangiwa, ikiwa ni pamoja na kuwapo madarasa, mabweni na walimu.

Lakini wanafunzi wa vijijini wakiwa wamepewa kipaumbele katika shule za kitaifa, kwa lengo la kuwajali wote ili wapate elimu bila kuwapo wanaobaki nyuma, kipindi hiki serikali ikigharamia elimu.

Kwa mujibu wa Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu, utaratibu wa kupanga nafasi hizo utasaidia wanafunzi walio kwenye mazingira magumu na vikwazo katika kupata elimu, ili wasome.

Ummy anataja idadi ya wanafunzi waliopangiwa shule za bweni za kitaifa kuwa ni 1,989, na kwamba wamechukuliwa zaidi wa vijijini, wakati kwenye majiji na halmashauri wameangalia zaidi wenye uhitaji tu.

Vilevile, waziri huo anataja wanafunzi wengine 4,188 ambao anasema ni wale walio na ufaulu bora zaidi, kwamba kuwa watapangiwa kulingana na alama zao kwa ujao wa mwaka 2022.

Pamoja na hayo, anatoa agizo kwa wakuu wa shule kote nchini kuacha visingizio vya michango au sare kwa wanafunzi wanaoanza bali waachwe waendelee na masomo huku mambo mengine yakiendelea kushughulikiwa.

Kwa ujumla utaratibu huo wa serikali unaweza kupunguza vikwazo ambavyo wanafunzi wa sekondari za vijiji wamekuwa wakikumbana navyo, ikiwamo kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

Hatua hiyo pia inaweza kuwaepusha na vishawishi vya njiani, ambavyo wakati mwingine vinaweza kusababisha waingie kwenye mahusiano na kujikuta wakipata mimba bila kutarajia na hata wavulana kujitumbukiza kwenye uhalifu. Aidha, utaratibu huo pia unaweza kuwafanya wakasoma masomo yote, kutokana na kwamba, shule nyingi za mijini zina walimu wa kutosha, tofauti na vijijini, hali inayosababisha wasome masomo machache.

Lakini, licha ya shule hizo kuwa na walimu wachache, hata hao wenyewe huwa wanataka wahame kwenda kwingine, hali ambayo imesababisha serikali kuingilia kati kwa kuzuia uhamisho huo. Waziri Ummy ameshapiga marufuku kuhamisha walimu kutoka katika halmashauri zilizoko pembezoni mwa nchi kabla ya kupeleka walimu mbadala, kuepusha changamoto zinazoweza kujitokeza kwa wanafunzi.

Katika kuhakikisha shule za vijijini zinakuwa na walimu wa kutosha, ameruhusu walimu kutoka mijini kwenda vijijini, badala ya kutoka vijijini kwenda mijini ambako kuna walimu wengi zaidi.

Anafafanua kuwa serikali imejikita katika kutoa elimu bora kwa jamii kwa kuhakikisha kunakuwa na mazingira bora ya kufundisha na kujifunzia na sasa inataka kuhakikisha kunakuwa na uwiano wa walimu, ili kutoa elimu sawa kwa watoto wote wa Kitanzania hasa katika halmashauri zilizoko pembezoni.

Hatua hiyo inayochukuliwa inaweza kumaliza mazingira hayo ambayo kwa namna moja au nyingine, hutajwa kukwamisha maendeleo ya kielimu ya wanafunzi wa shule za vijijini.

Kwa mbinu na utaratibu unaochukuliwa na serikali ninaamini kwamba, unaweza kufanikisha ndoto za wanafunzi wote katika elimu, kuanzia vijijini hadi mijini.

Ikumbukwe kuwa licha ya uhaba wa walimu katika shule za vijijini ambao husababisha baadhi ya masomo yasifundishwe, lakini unapofika wakati wa mtihani wa taifa wa kidato cha pili au cha nne, hulazimika kuufanya kwa masomo yote.

Hatua hiyo, inawezekana husababisha baadhi yao ambao hawakupitia katika vipindi vya masomo ya ziada 'twisheni', kufanya vibaya kwenye mitihani, kutokana na kwamba hawakuwa na msingi wa baadhi ya masomo.

Utaratibu huo mpya unaweza kuwa suluhisho la kikwazo hicho cha muda mrefu kwa wanafunzi wa shule za vijijini, ili waone utamu wa matunda ya elimu.

HABARI KITAIFA

# Corona ilivyoathiri tasnia ya habari

**Na Christina Mwakangale**

TASNIA ya habari imetajwa kuwa kati ya sekta iliyoathiriwa zaidi tangu kuwapo kwa corona, hasa kitaaluma, kisaikolojia na kiuchumi.

Kutokana na corona, baadhi ya wanataaluma walitakiwa kukaa nyumbani kutokana na kuyumba kwa uchumi kwenye baadhi ya vyombo vya habari.

Ofisa Programu wa Shirika linalojishughulisha na masuala ya utafiti, uhuru na haki za wanahabari liitwalo Article 19 kutoka Kenya, Sarah Wesonga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye semina ya waandishi wa habari kuhusu hali ya Covid-19 na tasnia hiyo.

Semina hiyo iliofanyika jijini Dar es Salaam, ilihusisha Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania (JOWUTA), Jumuiya ya Wanahabari Nchi za Kiafrika (CAJ) iliyoratibiwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Wesonga, alisema ripoti ya utafiti walioufanya, walibaini kuwa jumla ya waandishi wa habari watano Tanzania katika kipindi cha mwaka jana, wakati Covi-19 walifanyiwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Alisema serikali ya Tanzania ifanyie uchunguzi, ripoti zote za ukiukaji wa haki za binadamu dhidi ya waandishi wa habari na kuhakikisha wale wote waliotekeleza vitendo hivyo wanachukuliwa hatua za kisheria.

"Kutokana na vitendo hivyo tunaiomba serikali ya Tanzania kuchunguza ripoti zote za ukiukwaji wa wanahabari hao na kuwachukulia hatua za kisheria kulingana na viwango vya kimataifa wale wote watakaobainika kuhusika," alisema Wesonga.

Alisema, ni vyema serikali kuwalinda waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu na kwamba mashambulio dhidi yao hayakubaliki duniani kote, kwa lengo la kulinda uhuru wa kujieleza.

"Vitisho, mashambulizi, kupotezwa au kuuawa kwa waandishi wa habari kunachangia sio tu uhuru wa mtu kujieleza lakini unakiuka haki ya kuishi hata ya kiafya."

"Ndio maana tunatoa pendekezo kwa serikali kuchambua upya sheria zilizopo kuhusu uhuru wa kujieleza, ikiwamo hii ya uhuru wa vyombo vya habari kwa kuhakikisha zinalinda na haki za binadamu pamoja na Tamko la Umoja wa Afrika, kuhusu uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa habari," alisema Wesonga.

Naibu Katibu Mkuu JOWUTA, Said Mmanga, alisema kipindi cha corona kuliibuka taarifa 'feki' ambazo zilishusha weledi na tasnia ya habari nchini, ambazo nyingi zilitolewa kwenye mitandao ya kijamii. Alisema baadhi ya vyombo vya habari vililazimika kupunguza wafanyakazi wao, huku vingine vikishindwa kujiendesha kutokana na biashara kuzorota.

"Waandishi wa habari wakiendelea kutoa taarifa sahihi kuhusu suala la corona wataondoa sintofahamu iliyopo katika jamii kuhusiana na masuala ya Covid-19. Kipindi cha corona waliibuka waandishi mtandaoni wengi wasio na taaluma, hii ilifanya taaluma hii kupata wakati mgumu. Taarifa za uzushi, ukweli zilichanganywa.

"Tuendelee kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuchukua tahadhari kuhusiana na corona, tuwaeleze wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari," alisema Mmanga. Katibu wa CAJ, William Oloo, alisema taarifa za uwepo wa corona mwanzoni mwa mwaka jana, zilisababisha janga la kidunia na kuathiri mfumo wa maisha na kusababisha baadhi ya maeneo kukosekana njia sahihi za utolewaji wa taarifa hususani kuhusu ugonjwa huo.

Alisema ni jukumu la wanahabari kuhakikisha taarifa sahihi zinaifikia jamii ili kukabiliana na janga lililopo, na kwamba CAJ kwa kushirikiana na Chama cha Wanahabari Kenya (KCA), pamoja na Article 19, imebaini mradi kuongeza ufanisi wa kukabiliana na Covid-19 kwa nchi za Kiafrika na kwa kuhusisha nchi za Kenya, Tanzania na Ethiopia.

Alisema lengo la mradi ni kusaidia uhamasishaji baina ya asasi za kiraia, vyombo vya habari katika kuhakikisha sheria, sera na taratibu za utoaji wa taarifa sahihi za corona zinazingatiwa, ili kupunguza wingi wa habari 'feki' kuhusiana na athari na maambukizi ya ugonjwa wa Covid- 19.

## Adaiwa kujinyonga kisa kuzidiwa madeni

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Mmangawanga, Kata ya Kiwalala, Wilaya ya Lindi, Yahaya Hamisi Salum, anadaiwa kujinyonga hadi kufa kwa kilichoelezwa ni kuelemewa na madeni ya watu mbalimbali.

Inadaiwa wakati wa uhai wake Salum alipewa Sh. milioni 1.2 kwa ajili ya kununua mazao ya korosho na mpunga kutoka kwa wakulima mbalimbali kupitia mfumo usio rasmi maarufu kangomba, badala ya ule wa stakabadhi gharani kama ulivyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa taarifa zilizothibitishwa na ndugu wa marehemu na viongozi wa serikali ya kijiji na kata, mtu huyo alijinyonga kwa kutumia kamba ya manila katika shamba la baba yake mzazi aitwaye Hamisi Salum.

Aidha, mwili wake uligunduliwa na mama yake mdogo aitwaye Zuhura Dadi, Novemba 25 mwaka huu, 2021.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Dada wa marehemu, Asha Juma alithibitisha mdogo wake kujinyonga baada ya kuwaaga ndugu zake kuwa anasafiri kwenda wilayani Masasi, mkoani Mtwara kumtembelea kaka yao.

"Salum alimuaga mama yetu mzazi kuwa anaenda Masasi kumtembelea kaka yetu mwingine na angerejea siku hiyo hiyo, lakini hakurudi tulipata hofu tukawapigia ndugu zetu bila mafanikio. Wakati mama mdogo anaenda shambani kwake akamwona kwa mbali an 
ning'inia kwenye shina la mkorosho," alisema.

Alisema aliwajulisha ndugu ambao walikwenda eneo la tukio na kujiridhisha kuwa amejingonya na ameshafariki, na kwamba walitoa taarifa kwenye mamlaka kisha polisi walifanya uchunguzi na kuruhusu wazike.

Baadhi ya wananchi wa karibu walidai kuwa kifo hicho kilitokana na kuzidiwa na madeni ya watu aliahidi kwenda kuwanunulia korosho na mpunga kwa utaratibu usio rasmi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji husika cha Mmangawanga, Ahamadi Ally na Ofisa Mtendaji Kata ya Kiwalala, Zaituni Lichinga, walithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba sababu ya kifo ni mtu huyo kujinyonga.



Viongozi wastaafu wa Chama cha Kuweka na Kukopa Kimalela Saccos wakifurahia jambo baada ya kutunukiwa vyeti vya utendaji katika chama hicho, halfa iliyofanyika katika mkutano mkuu wa mwaka jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## PM ataja sababu ujenzi vyuo vya ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imefanya uamuzi wa kujenga vyuo vya ufundi stadi nchini ili wananchi hususani vijana wapate ujuzi wa ufundi wa aina mbalimbali utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Alitoa kauli hiyo jana, baada ya kukagua na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, na kuagiza ujenzi huo ukamilike kwa wakati ili malengo ya serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya ufundi chuoni hapo yanafikiwa.

Alisema serikali imeamua kujenga vyuo hivyo vya ufundi stadi ili kufungua milango ya ajira kwa kuwa mafunzo yanayotolewa yatawawezesha wahusika kujiajiri katika sekta mbalimbali ikiwamo ya viwanda.

"Ninawaomba wananchi mwendelee kuwa na imani na serikali yenu."

Kadhalika, Waziri Mkuu ameuagiza uongozi wa mkoa wa Mbeya uhakikishe katika eneo hilo la kijiji cha Mbugani kinapojengwa chuo hicho kunakuwa na huduma zote za kijamii zitakazotosheleza matumizi ya eneo hilo zikiwamo za majisafi na salama na umeme.

Pia alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawasihi wananchi waendelee kuyalinda maeneo yao yaendelee kuwa tulivu ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. "Suala la kuimarisha ulinzi na usalama ni jukumu la wananchi wote, hivyo tuendelee kushirikiana katika kuimarisha ulinzi," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Dk. Pancras Bujulu, alisema mradi huo una jumla ya majengo 17 ambayo ni jengo la utawala, karakana nne, jengo la madarasa, mabweni mawili, bwalo la chakula, majengo matatu ya vyoo, nyumba ya mkuu wa chuo, nyumba ya familia mbili za watumishi, jengo la mitambo ya umeme, jengo la stoo na jengo la walinzi.

Alisema chuo hicho kitakapokamilika kinatarajiwa kuanza na fani sita za muda mrefu, nazo uhazili na kompyuta, ushonaji na ubunifu wa mitindo, uashi, umeme wa majumbani, ufundi magari pamoja na uchomeleaji na uungaji wa vyuma. Amesema gharama za ujenzi wa chuo hicho ni shilingi bilioni 1.6.

# Kilombero kuwekeza bil. 700/- kukabili uhaba wa sukari nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMPUNI ya Sukari ya Kilombero, inatarajia kuanza mradi wake wa upanuzi ambao utakuza mchango katika ukuaji wa uchumi kutoka Sh. bilioni 340 za sasa hadi kufikia takribani Sh. bilioni 700 kwa mwaka.

Mradi huo wa upanuzi utakaohitaji uwekezaji mpya wa awali wa zaidi ya Sh. bilioni 550, unajumuisha kiwanda kipya kitakachokuza uwezo wa kampuni hiyo wa kutengeneza sukari na kupunguza uhaba nchini kupitia chapa yake ya "Bwana Sukari".

Mkuu wa mauzo wa kampuni hiyo, Ephraim Mafuru, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma katika mkutano wa 20, wa taasisi za kifedha nchini.

Mafuru, alisema hiyo ni miongoni mwa mikakati ya kampuni hiyo kufikia maono yake ya kupunguza utegemezi wa nchi katika bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa inajitosheleza katika uzalishaji wa sukari ifikapo 2025.

"Mradi wetu wa upanuzi utakuza uzalishaji wa sukari kutoka tani 126,000 hadi tani 271,000 kwa mwaka hivyo kuisaidia serikali kuokoa takribani dola za Kimarekani milioni 70, katika uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi," alisema Mafuru.

Mafuru aliongeza kuwa upanuzi huo unatarajiwa kukuza kiwango cha miwa kinachonunuliwa kutoka kwa wakulima ifikapo 2026/27 kwa takribani tani milioni moja kwa mwaka zaidi ya tani 600,000 zinazonunuliwa sasa na hivyo kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo na uboreshaji wa miundombinu ya maendeleo na huduma za kijamii katika jamii zilizo jirani na kiwanda hicho. Aidha, alisema kampuni ya sukari ya Kilombero imedhamiria kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua uchumi ulioporomoka kutokana na janga la UVIKO-19.

"Pamoja na kukuza mchango wetu katika ukuaji wa uchumi, upanuzi huo utazalisha fursa za ajira za kudumu 2,000 na ajira 2,440 za mikataba, pamoja na kuzalisha Megawati 10 hadi 15 za umeme wa nishati mbadala zinazoweza kuingizwa kwenye gridi ya taifa kupitia mkataba wa ununuzi wa umeme (Power purchase agreement - PPA) na TANESCO," alifafanua.

"Ujio wa UVIKO-19 kwa kiasi kikubwa umeyumbisha ukuaji wa uchumi kote duniani. Kiwanda chetu kipya kitawezesha kwa kiasi kikubwa kuunga mkono mkakati wa serikali wa kufufua uchumi, hasa kupitia ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi wa viwanda.

"Ni dhamira yetu kuendelea kuchangia katika kuboresha maisha ya jamii zinazotuzunguka na kukuza uchumi wa nchi kwa kuongeza mapato ya wakulima, kuongeza mapato ya serikali, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi, sambamba na kujenga thamani ya muda mrefu kwa wadau wetu wote," alisema Mafuru.

Mradi huo wa upanuzi utanufaisha sekta mbalimbali, ukiwamo ujenzi, kilimo, viwanda na usafirishaji.

Kampuni ya sukari ya Kilombero, inamilikiwa na kampuni ya Illovo Sugar Africa kwa asilimia 75 na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 25.



Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, Abdallah Malela (watatu kushoto), akimkabidhi zawadi ya guta mmoja wa washindi wa droo ya nne ya kampeni ya Vuna Zaidi na NBC Shambani inayoendeshwa na Benki ya NBC mahususi kwa wakulima wa korosho mikoa ya Lindi na Mtwara, Ally Ismail ambaye ni Katibu Mkuu wa AMCOS ya Tangazo mkoani Mtwara wakati wa hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa kampeni hiyo, iliyofanyika mkoani Mtwara mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni Meneja wa Benki hiyo Kanda ya Kusini, Zubeider Haroun (kushoto) na Meneja wa Benki hiyo tawi la Mtwara, Editha Mwakatobe (wa pili kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# CCM yaingilia kati sakata wastaafu 300 kusotea mafao

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) makao makuu kupitia ziara ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu kimepokea malalamiko ya walimu wastaafu 300 ambao kwa zaidi ya miaka minne wamekuwa wakisotea malipo yao ya nauli na malipo ya kusafirishia mizigo yao baada ya kustaafu.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, alibainisha hayo mkoani Geita kwa wanahabari wakati akitoa tathmini ya ziara ya kikazi ya sekretarieti hiyo kutembelea mikoa yote kwa lengo la kuainisha uhai wa chama na kero na kubaini changamoto ikiwemo ya walimu aliyoiita bomu.

Alisema idadi kubwa ya orodha iliyopokewa makao makuu mengi ni kutoka Manispaa ya Temeke na mkoa wa Rukwa ambapo mikoa mingine ukiwamo Mwanza ilikuwa mbioni kuwasilisha madai hayo.

Ambapo wametakiwa wenye malalamiko ya ina hiyo nchi nzima kuyawasilisha mara moja ili yafanyiwe kazi.

"Mpaka jana CCM makao makuu tulikuwa tumepokea malalamiko ya wastaafu 300, hawa wote ni walimu ambao wamekuwa wakisotea madai yao ya nauli zao na mizigo yao kwa zaidi ya miaka minne bado hawajaambulia kitu, hii ni hatari kwa mustakabali wa taifa," alisema Lubinga.

Aliwashauri wastaafu wengine wote wa umma wenye kero za madai ya aina hiyo waziwasilishe kwenye ofisi za wilaya na mikoa za CCM ambazo zitayafikisha malalamiko hayo kunakohusika.

Akionekana kukerwa na malalamiko hayo, Kanali Lubinga alisema inashangaza serikali kutenga bajeti kila mwaka ikiwemo malipo ya nauli za wastaafu pamoja na za kusafirisha mizigo yao baada ya kustaafu, lakini wanapata tabu kulipwa.

Lubinga ameelekeza wakurugenzi wote wa halmashauri nchini kupitia TAMISEMI kuhakikisha wanalipa madai hayo, na kwamba maelekezo hayo yatakabidhiwa kwa serikali kupitia kwa waziri mwenye dhamana.

# W/biashara wasiotoa risiti za EFD kukiona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania(TRA) Mkoa wa kikodi Kahama, imewataka wafanyabiashara wilayani hapa kuhakikisha wanatoa risiti za mashine za kielektroniki (EFD) kwa wateja wao ili kuondokana na migogoro ambayo imekuwa ikijitoza wanapobainika kutotoa risiti.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa TRA Kahama, Waliyoba Kanire, wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake juu ya hatua ambazo mamlaka imekuwa inazichukua pale inapobaini baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa na tabia ya kutokutoa risiti za EFD kwa wateja wao.

Alisema Oktoba mwaka huu waliwafikisha mahakamani wafanyabiashara 12 kwa tuhuma za kutotumia vema na kutoa risiti za EFD, huku baadhi yao wakiwa na tuhuma za kushindwa kuitikia wito wa TRA, na kwamba hatua hiyo imewafanya wasitumia mashine hizo ipasavyo.

"Kazi yetu sisi TRA ni kutoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara wetu na kukusanya maduhuri ya serikali, tunapotoa elimu juu ya matumizi sahihi ya EFD na wasiyafuate lazima mwisho wa siku tuwachukulie hatua za kisheria ili serikali isiendelee kupoteza mapato yake," alisema Kanire.

Aliongeza: "Niwahimize wafanyabiashara wetu tutimize wajibu wetu wa kutoa risiti kwani kwa wateja wetu... kutumia mashine za EFD kwa usahihi hakuongezi kodi TRA na utakuwa umekwepa adhabu zitakazoweza kudumaza biashara yako."

Aidha, Kanire alisema kuwa muuzaji asiyetoa risiti kwa mteja wake adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. milioni tatu na isiyozidi Sh. 4,500,000 au kifungo kisichozidi miaka mitatua jela au vyote kwa wakati mmoja, hivyo kuwataka kuwa mabalozi wazuri wa matumizi ya mashine hizo.

Naye Mkaguzi wa Kodi kutoka TRA, Irene Hance, alisema kabla ya kuanza kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaokwepa kutumia mashine na kutoa risiti kwa wateja wao huwa wanaanza kwa kutoa elimu juu ya umuhimu wa kodi ili wanapowachukulia hatua wasilalamike popote.

Aidha, alisema baada ya kuwafikisha katika vyombo vya sheria takribani wafanyabiashara 12 kwa makosa ya kutotumia mashine hizo, kwa sasa hali imeanza kubadilika kwani wengi wao wameanza kutoa risiti hizo ikiambatana na elimu wanaoyoitoa kwao.

Mmoja wa wafanyabiashara waliofikishwa mahakamani kwa tuhuma za kutotoa risiti za EFD kwa wateja, James Ndeki, alikiri kosa mbele ya Mahakama kwa kutokutumia na kutoa risiti kwa wateja wake na alitozwa faini, hali iliyomfanya abadilike na kwa sasa amekuwa balozi wa kupinga wasiotumia EFD.

# DC Masasi aonya wazazi wasiopeleka watoto shule

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Claudia Kitta, amewaonya wazazi watakaozuia watoto wao waliofaulu kuendelea na kidato cha kwanza mwaka 2022, kuwa watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara kwenye vijiji mbalimbali kukagua shughuli za maendeleo.

Alisema serikali ina jukumu la kuhakikisha uwapo wa miundombinu ili kila mwanafunzi apate pa kusomea na kuondoa visingizio na ndiyo maana mwaka huu kuna mikakati ya kuhakikisha wanafunzi wote wanaingia kwa mkupuo.

Kwa mujibu wa Kitta, ni wajibu wa kila mzazi kuhakikisha mwanaye aliyefaulu anakwenda katika shule aliyopangiwa na siyo kuwazuia kwa kuwa iko makini inafuatilia kila mwanafunzi.

Alisema wazazi wanapaswa kutumia kwa malengo fedha za korosho wanazoendelea kupokea kwa kujiwekea akiba na kununua mahitaji ya msingi ya watoto wao, ikiwamo kuwapeleka watoto wao shuleni, kuwanunulia sare na mahitaji mengine ya msingi ya shuleni ili watoto waweze kusoma.

"Nitoe rai kwa wazazi na walezi wote wilayani hapa ambao watoto wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani kuhakikisha watoto hawa wanakwenda shuleni na hakuna atakayebaki nyumbani, tutachukua hatua kwa atakayeshindwa kumpeleka mtoto wake shuleni," alisema Kitta.

Mkuu huyo wa wilaya alisema serikali haitokubali kuona mtoto amechaguliwa kwenda sekondari halafu anakaa nyumbani kwa sababu mzazi ameshindwa kumpeleka shuleni eti kwa ajili ya mzazi au walezi kukosa fedha za kumsomesha mtoto wake, mzazi kama huyo lazima afikishwe kwenye vyombo vya kisheria kujibu hoja hiyo.

"Naagiza wenyeviti wa vitongoji, mitaa na watendaji wa vijiji na kata kuhakikisha wanawatambua watoto wote waliomaliza darasa la saba na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ili wazazi wakishiriki mbinu mbaya wajulikane kirahisi,"alisema.

Kwa mujibu wa DC huyo, baadhi ya wazazi hawaipi elimu kipaumbele kiasi cha kuwataka watoto wao wanapofanya mtihani wa darasa la saba kutofanya vizuri ili kukwepa kumsomesha bila ya kujua elimu ni urithi wa mtoto kwa maisha yake ya baadae.

Mkazi wa kijiji cha Mbuyuni, Mohamedi Bakari alimpongeza kiongozi huyo kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wazazi kuona umuhimu wa elimu kwa watoto wao ikiwamo ujenzi wa miundombinu muhimu.

# Mgombea ubunge wa CCM Ngorongoro aahidi kiwanda

**Na Thobias Mwanakatwe,** NGORONGORO

MGOMBEA ubunge katika uchaguzi mdogo Jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha, Emmanuel Shangai kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), amesema iwapo wananchi watampa ridhaa ataishinikiza serikali iweze kujenga kiwanda cha kusindika nyama.

Akizungumza na wananchi kwa nyakati tofauti katika mwendelezo wa kampeni zake kwenye kata za tarafa ya Sare,Ngorongoro na Loliondo, alisema atashinikiza ujenzi wa kiwanda hicho kwa wananchi ambao asilimia kubwa ni wafugaji katika jimbo hilo waweze kupata soko la uhakika la mifugo yao.

Kuhusu chanjo ya mifugo, alisema katika kipindi cha uongozi wake atahakikisha mifugo inapewa chanjo wakati wa masika badala ya hivi sasa mbapo chanjo hiyo inatolewa kipindi cha kiangazi ambapo mifugo imekuwa ikifa kwasababu kunakuwa hakuna malisho mazuri.

Shangai alisema mambo mengine atakayohakikisha yanatekelezwa katika jimbo hilo ni ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo ujenzi wake ulishaanza lakini haujakamilika na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Ngorongoro ambacho kinajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 3.

Alisema ujenzi wa chuo hicho umeanza tangu mwaka jana lakini haujakamilika ambapo serikali ilishatoa fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.5 kati ya bilioni 3 zinazotakiwa kutolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo.

Shangai alisema jambo jingine atakalohakikisha linapatiwa ufumbuzi ni ujenzi wa barabara ya kutoka Mto wa Mbu hadi Loliondo kwa kiwango cha lami. Alisema barabara hiyo ambayo ni muhimu sana kiuchumi, ujenzi wake ulishaanza na zimejengwa kilometa 49 tu bado kilometa 243 ambazo atahakikisha anaishinikiza serikali imalizie ujenzi huo ili kuwarahisishia wananchi usafiri kwani wamekuwa wakipata changamoto sana wakati wa masika.

Aidha, alisema changamoto za uboreshaji wa miundombinu ya elimu na maji ni miongoni mwa kero ambazo atahakikisha zinapatiwa ufumbuzi katika jimbo hilo.

Aliwaomba wananchi wamuunge mkono kwa kumchagua ili aendeleze kutekeleza miradi inayoendelea kujengwa na serikali ya CCM katika jimbo hilo.



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Kundo Andrea (kushoto), akizindua maabara ya TEHAMA kwa Chuo Kikuu cha Dodoma iliyotolewa kwa msaada wa Kampuni ya Huawei wakati wa hafla fupi iliyofanyika jijini Dodoma jana. Wanaotazama ni Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Leonard Mselle (kulia), Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Huawei, Tom Tao (wa pili kulia). **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Huawei yaipiga jeki UDOM vifaa TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Huawei Tanzania imetoa msaada wa maabara ya TEHAMA kwa Chuo Kikuu cha Dodoma ikiwa na nia ya kuibua mawazo ya kibunifu na kuboresha sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano nchini.

Maabara hiyo ina miundo msingi ya kisasa na ambayo inaweza kuwasaidia wanafunzi kupata ujuzi halisi wa vitendo unaohitajika katika mapinduzi ya nne ya viwanda. Kwa zaidi ya miaka miwili, Huawei imekuwa ikishirikiana na UDOM katika masuala ya TEHAMA hasa katika kujenga uwezo na usimamizi wa maarifa ikiwa ni sehemu ya mchango wa kampuni hiyo katika maendeleo ya taifa.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa maabara hiyo inayojulikana kama Huawei ICT Lab katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Mhandisi Kundo Andrea, alipongeza Huawei kwa maabara hiyo akisema kuwa ni hatua kubwa kuelekea mabadiliko ya kidijitali nchini.

Alisema kwa kuwekeza kwenye TEHAMA, kwa wabia hao wawili imekua ni chachu ya ukuaji wa uchumi wa nchi kwani kuwekeza katika sekta hiyo ni muhimu kwa kuzingatia dira ya maendeleo ya 2025.

"Pongezi kubwa kwa Huawei kwa kufanikisha mpango huu muhimu. Tangu kuanzishwa kwake nchini Tanzania miaka 13 iliyopita, Huawei imekuwa na mchango mkubwa katika kutoa mafunzo na kulea wanafunzi wa ndani wa TEHAMA kupitia programu yake maarufu ya Huawei ICT Academy iliyoanzishwa mwaka 2018," alisema na kuongeza:

"Wizara itaendelea kushirikiana na Huawei kuongeza uelewa wa TEHAMA, kuweka miundombinu ya TEHAMA, na kutoa maudhui na ujuzi kwa wanafunzi kote nchini'."

Mbali na maabara ya TEHAMA ya UDOM-Huawei, Naibu Waziri alizindua maabara za ukarabati na matengenezo ya simu za mikononi. Alisema UDOM ni mfano wa wazi wa taasisi zilizowekeza kwa dhati katika TEHAMA.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Huawei, Tom Tao, alisema kampuni yake imedhamiria kuwekeza katika kizazi kipya kwa kuwapa ujuzi muhimu unaoweza kusaidia nchi kupata maendeleo kupitia teknolojia ya kidijitali.

"Kipaumbele chetu ni kukuza vipaji vya vijana hasa katika tasnia ya ICT ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi na kizazi cha vijana kimeonekana kuwa rasilimali yenye ushawishi kwa nchi," alisema Tao.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, aliwataka walengwa wa Maabara hiyo kuitumia ipasavyo kwa maendeleo ya nchi.

"Sote tunafahamu lengo la nchi la kufikia uchumi wa kidijitali, katika kufikia lengo hilo nchi inahitaji wataalamu wenye ujuzi wa TEHAMA," alisema Dk. Akwilapo.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Leonard Mselle, aliishukuru Kampuni ya Huawei Technologies kwa kuwa mstari wa mbele siku zote katika kuchangia kuwajengea uwezo vijana wa Kitanzania.

# Serikali yasema imedhamiria kumaliza migogoro ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SERIKALI imesema imedhamiria kumaliza kero na migogoro ya ardhi nchini kwa kutatua iliyopo na kuweka mikakati ya kuzuia migogoro mipya ikiwemo utwaaji maeneo ya wananchi bila kulipa fidia

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, mwishoni mwa wiki jijini Mwanza wakati wa kutatua migogoro ya muda mrefu ya ardhi iliyopo Wilaya ya Nyamagana ukiwamo mgogoro wa wananchi na mwekezaji Kampuni ya Pamba Engineering uliopo Kata ya Mhandu.

Mgogoro mwingine ni kati ya msimamizi wa mirathi Ndugu Abuu mwana familia ya marehemu Mzee Seif eneo la Miembeni mtaa wa Nera kata ya Isamilo kuhusu umilikishwaji eneo lao la urithi na ulipwaji fidia kwa wananchi wa mtaa wa Kisoko katika kata ya Luchelele kutokana na serikali kutwaa eneo lao kwa ajili ya ujenzi wa shule

Katika kutatua mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji Pamba Engineering, Mabula ameelekeza wananchi kumilikishwa eneo linalolalamikiwa kati yao na mwekezaji katika kata ya Mhandu kufuatia wananchi hao kukidhi matakwa yote ya kisheria na kulipa gharama za umilikishaji huku familia ya marehemu Mzee Seif ikielekezwa kupatiwa viwanja saba vilivyopatikana baada ya kupimwa eneo lao la asili alilolinunua marehemu baba yao miaka ya themanini kwa aliyeteuliwa kusimamia mirathi baada ya kujiridhisha

Kuhusu eneo la mtaa wa Kisoko kata ya Luchelele, Mabula mbali na kuwataka wananchi wa mtaa huo kushirikisha viongozi waliopo katika maeneo yao kutatua kero mbalimbali za ardhi, alimwelekeza Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Sekiete Yahaya, kuhakikisha anawalipa fidia wananchi wote 20 waliotwaliwa maeneo yao na serikali kwa ajili ya ujenzi wa shule mapema kabla ya mwaka wa fedha 2021/2022 kuisha ambapo kiasi cha shilingi milioni 350 zinadaiwa na wananchi hao

"Nikuombe Mkurugenzi, wananchi hawa wamekaa muda mrefu wakisubiri fidia wengine wameshindwa hata kuendeleza maeneo yao kwa sababu hawajalipwa fidia, naomba wananchi hawa walipwe wote kabla ya mwaka wa fedha wa sasa kuisha," alisema Dk. Mabula.

Kwa upande wake, Yahaya alisema maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya taasisi za serikali kama shule na huduma nyengine yatalipwa fidia kwa awamu mpaka deni lote litakapokwisha.

"Mhe Naibu Waziri naahidi kulipa fidia kwa awamu kuanzia kipindi hiki cha kati kati ya mwaka wa fedha 2021/2022 na kumaliza jumla ya milioni 150 kufikia mwishoni mwaka huu wa fedha" alisema Yahaya.

Naye Diwani wa Luchelele, Vicent Lusana, alifafanua kuwa wanafunzi wanaotoka eneo lake wamekuwa wakitembea umbali mrefu kwa ajili ya kufuata elimu na kusisitiza kuwa ipo haja kwa serikali kuharakisha ulipwaji wa fidia ili waanze ujenzi wa shule kwa lengo la kuwawezesha wanafunzi wa eneo hilo kupata elimu katika umbali mfupi na kuwaepusha na changamoto mbalimbali ikiwemo mimba za utotoni

Kamishina wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Mwanza, Elia Kamihanda, alitaka kuzingatiwa utengwaji maeneo kwa ajili ya shughuli za umma katika upimaji na upangaji wa mji, huku akiwataka wananchi kuhakikisha wanayalinda maeneo yote yanayotengwa kwa matumizi ya jamii.




Mabalozi wa usalama barabarani (RSA) kutoka baadhi ya mikoa nchini, wakitembelea eneo la kumbukumbu ya ajali ya wanafunzi 32 na wafanyakazi watatu wa Shule ya Lucky Vincent iliyotokea Mei 6, 2017 katika kilima cha Rotya wilayani Karatu mkoani Arusha, kuadhimisha Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani. **PICHA: ROSE JACOB**

## Wahitimu vyuo vikuu waitiwa ajira serikalini

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAHITIMU wa vyuo vikuu wametakiwa kuamini kwamba ajira serikalini bado zipo hivyo wazitafute badala ya kukata tamaa wanapohitimu masomo yao na kushindwa kujishughulisha.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Mwanza na Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Dotto James, katika mahafali ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Alisema wasomi wengi kwa sasa wamekata tamaa kwa kudhani kwamba hakuna ajira za serikali, jambo ambalo siyo kweli.

Aliongeza kuwa ajira serikalini zipo japokuwa ni chache, hivyo wasomi wafikirie kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea kuajiriwa.

"Kazi ndani ya serikali bado zipo ingawa ni chache, wasomi wasikate tamaa, lakini pia kuna ajira za kujiajiri wenyewe na kuajiri wenzao," alisema James.

Aliongeza kuwa wasomi hao baada ya kuhitimu wanatakiwa kufikiria namna ya kujiajiri ama kuajiriwa badala ya 'kubweteka'

"Alikiomba chuo hicho kuandaa mpango maalumu wa kuwapatia semina wahitimu waliosoma chuoni hapo kuhusu namna bora ya kujiajiri badala ya kutegemea ajira," alisema.

Aidha, James aliahidi kufikisha kero mbalimbali zinazokikabili chuo hicho kwa serikali Ili kuzipatia ufumbuzi.

Kero hizo ni pamoja na kukosekana kwa umeme wa uhakika pamoja na ubovu wa barabara inayoingia chuoni hapo.

Kwa upande wake, Mkuu wa chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema, alisema, kwa sasa idadi ya wanafunzi imeongezeka.

Alisema chuo hicho kilianzishwa mwaka 1965 kikiwa na idadi ndogo ya wanafunzi, lakini leo imeongezeka na kwamba Mwanza pekee ina wanafunzi 2,000.

Aliongeza kuwa jumla ya wahitimu 440 walitunukiwa vyeti kwa ngazi ya cheti, stashahada na shahada katika kozi mbalimbali.

# Ujenzi wa madarasa wamkosha Waziri Dugange

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, ameipongeza Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara kwa kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 35 kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022.

Alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kikazi wilayani Masasi alikojionea kasi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na uwepo wa vifaa vyote muhimu.

Akiwa kwenye ziara hiyo, alitembelea na kujionea ujenzi wa madarasa shule ya sekondari ya wasichana Masasi, sekondari ya kutwa ya Anna Abdallah, ujenzi wa kituo cha afya cha Mtandi kilichopewa Sh. milioni 250.

"Nimeridhishwa na ujenzi unaoendelea na kuona namna fedha za serikali zinatumika, kazi iliyofanyika ni nzuri ni muhimu ikaendelea ili kufikia malengo husika," alisema. Dk. Dugange alisema kutokana na kasi hiyo inaonyesha nia ya serikali ni kutokuwa na awamu mbili za wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa itafikiwa kwa kuwa wote wataingia darasani kwa wakati mmoja.


Aidha, alisema Halmashauri ya mji Masasi ilipokea Sh. milioni 820 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 35 katika shule zake mbalimbali za sekondari.

Alisema kwa upande wa sekondari ya wasichana Masasi pamoja na sekondari ya kutwa ya Abdallah kila moja imepata Sh. milioni 80 kwa ajili ya kujenga madarasa manne kwa kila shule.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema wadau wote muhimu wameshirikishwa kuhakikisha ujenzi huo unakwenda kwa kasi na kwamba matarajio ni kukamilisha kabla ya muda uliopangwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya mji Masasi, Elias Ntiryhungwa, alisema halmashauri imepokea jumla ya Sh. milioni 820 za ujenzi wa madarasa 35 na Sh. milioni 250 za ujenzi wa kituo cha afya Mtandi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 30, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## Wafugaji ‘mnafeli hapo’



Ukurasa 13

## Wadau: Masomo baada ya uzazi

ELIMU

NA DINNA MANINGO, TARIME

HALMASHAURI ‘SOMA HIYO’…

# Mikopo kwa wanawake na vijana, pasipo kinababa, inakwamisha elimu

UNAWEZA usiamini lakini ndiyo madai ya wajasiriamali wanaosindika ngozi, wanaoonya kuwa utaratibu wa kutoa fedha za mikopo kwa vijana, kinamama na watu wenye ulemavu bila wanaume ni sawa na kutoa mitaji isiyoleta maendeleo.

Wanaiambia Nipashe utaratibu unaowabana na kuwakataa wanaume wenye miaka zaidi ya 35 wanaotamani kukopa, lakini hawawezi tofauti na wanawake ambao hawana ukomo wa umri, hawaufurahii, kwa sababu baba angepata mkopo angesaidiana na mama kusomesha watoto.

Wanadai sera hiyo ya mikopo kwa vijana haimgusi wala haimruhusu mwanaume mwenye zaidi ya miaka 35 kupata mikopo inayotolewa na serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri, inawashangaza.

Wanaume wanaochakata ngozi na watengenezaji wa bidhaa za ngozi wasio vijana wa umri huo wanasema wameshindwa kujiinua kiuchumi na kuwa wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa hiyo kwa kuwa wanatumia teknolojia duni zisizokuwa na ubora hali inayokolezwa na kukosa fedha za kununua vitendea kazi vya kisasa.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wanaume wilayani Tarime mkoani Mara, ambao wanajihusisha na utengenezaji wa bidhaa za viatu vya ngozi wanasema maelekezo ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu pekee ni ubaguzi unaozidi kuziweka baadhi ya familia za wanaume kwenye umaskini, kisa tu si vijana.



Bidhaa za ngozi zinazozalishwa na kutawala soko hivi sasa. **PICHA: MTANDAO.**

Umaskini huo unarudisha nyuma elimu kwa watoto ambao wengine hukosa ada kutokana na familia kukosa mapato.

Magala Masatu (51), anajishughulisha na utengenezaji wa viatu vya ngozi, akifanya kazi zake mtaa wa National Housing, mjini Tarime anasema:

“Kitendo cha wanaume kutopewa mikopo ya serikali kimenikwamisha kimtaji na kunisababishia kuendelea kutumia njia za kizamani kutengeneza viatu na hivyo kujikuta nikitumia muda mrefu bila mafanikio.”

“Sera ya kutoa mikopo kuwagusa wanawake, vijana na walemavu pekee inatuumiza wanaume watu wazima. Wanawake hawabaguliwi hawana ukomo. Sisi serikali imetutenga na kutubagua japo tunachangia sana katika kukuza pato la taifa kupitia shughuli mbalimbali zinazotumia nguvu za wanaume.”

Anaongeza: “Natumia mikono kukandamiza soli ninapotengeneza viatu, naipitisha kwenye moto ili kuilainisha, unapotumia mikono pekee bila mashine inakuchukua muda mwingi kutengeneza kiatu, kwa siku unatengeneza pea moja ya. Ningekuwa na mtaji wa halmashauri haya yasingetokea ningenunua mashine.”

“Tungekuwa na vitendea kazi vya kisasa uzalishaji ungeongezeka na ubora pia. Ningenunua mashine za kupunguza unene kwenye maungio ya viatu na kukandamiza kiatu kishikane ingenirahisishia kazi zaidi,” anasema Masatu.

Mwanaume huyu anasema wenye umri wa makamo (zaidi ya miaka 40) kama yeye mtaji wake ni mdogo haujamwezesha kununua vitendea kazi vya kisasa zikiwamo mashine za kisasa na kwamba anaogopa kukopa benki kutokana na riba kubwa na masharti magumu, lakini kama ingekuwa ni mkopo wa halmashauri angefanikiwa.

“Mtaji wangu ni Shilingi 2,000,000 wakati mashine ni zaidi ya 3,000,000 kulingana na mahitaji ili biashara yako iwe bora na mzunguko mzuri inatakiwa uwe na mtaji angalau Sh. milioni 10, mikopo ya benki ina riba kubwa. Kuna mingine ukikopa 100,000 unatakiwa kurejesha 130,000-140,000 na mingine unakopa 300,000 unawasilisha hati ya mali isiyohamishika. Inawezekana nyumba yako ikanadiwa kwa kiasi kidogo cha fedha na kukuongezea umaskini zaidi si wewe tu hata familia na pengine ukoo unaokutegemea.

### WANAUME TUNAUMIA

“Tunaipenda mikopo ya serikali ni mizuri haina riba kubwa, lakini inatolewa kwa ubaguzi na sisi wanaume tunaozidi miaka 35 hatupewi nafasi. Mikopo isiwe tu kwa vijana, inatolewa kwa wanawake bila kujali ni mzee au kijana, haina mipaka ya umri, wanaume tukipewa mikopo itatuinua kiuchumi,” anasema Mwilole Mwita.

Mwita mtengeneza viatu vya ngozi anasema malighafi za kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi zina gharama kubwa na kwamba akipewa mkopo usio na riba atafanikisha biashara yake ya viatu na mazao mengine na kumwinua kuliko kubakia kama alivyo.

“Natengeneza bidhaa zote zitokanazo na ngozi kama viatu, mabegi, mikoba, mikanda na nyinginezo, lakini kwa kuwa mtaji ni mdogo nimejikita kwenye viatu vya ngozi ya ng’ombe na mbuzi zilizochakatwa na kiwanda cha Moshi. Zamani tulikuwa tunachukua ngozi maduka ya Mwanza...” anasema Mwita.

Anaongeza kuwa: “DIT Mwanza wana kiwanda cha ngozi lakini hajazitumia huku akitamani zinazotoka nje kwa maelezo kuwa zina ubora zaidi ikilinganishwa na za hapa nchini na kwamba bei ya ngozi ya ndani ikishuka na za viatu itashuka pia,” anasema Mwita.

Mwita Marwa (58), mkazi wa Kijiji cha Matongo anasema wanaume wenye umri zaidi ya miaka 35 ndiyo wanaoongoza kumiliki mifugo mingi

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA
NA MWANDISHI WETU

## NDEGE MPYA YA UMEME HII HAPA…

# Ina kasi kuliko sauti, salama kwa mazingira

KUNA msemo kuwa hakishindikani kitu tena hakuna kuchoka mpaka kieleweke, ndivyo kampuni ya Rolls-Royce ilivyofanya.

Pengine ndivyo Rolls-Royce kampuni ya Uingereza ilivyoounda, ni baada ya kuunda ndege ya umeme inayoweka rekodi ya mwendo kasi mkali duniani ikipewa jina la 'Spirit of Innovation' au Roho ya Ugunduzi.


Ndege hiyo inasafiri kasi ya kilomita 623 kwa saa wakati wa majaribio, ikitumia betri badala ya mafuta na kuandika upya historia ya safari za anga zisizochafua mazingira na kuongeza mabadiliko ya tabianchi.

Rolls-Royce inasema baada ya mafanikio ya safari ya kuunda ndege yenye kasi kubwa tena inayotumia betri kikamilifu, mazungumzo yameanza kuhusu usafiri wa anga wa kielektroniki.

Mafuta ya visukuku (mabaki ya wanyama na mimea yaliyofunikwa ardhini kwa miongo mingi) yanayotumika kwenye injini za ndege na kutoa kaboni kwa wingi na kuchafua angahewa, yanalazimika kufikia upeo kwani huongeza joto dunia.

Mwanasayansi katika Chuo Kikuu cha South Carolina nchini Marekani, Tanvir Farooq - ambaye anatafiti teknolojia ya anga - anasema 'Sprit of Innovation' imethibitisha uwezekano wa ndege kuruka kwa kutumia umeme.

Anasema, lakini bado kuna mashaka juu ya jinsi ndege kama



hiyo inavyoweza kuruka kwa kasi.

**FAROOQ ANAONGEZA:**

"Ni ndege inayotumia propela, ina kikomo cha kasi fulani. Kwa ndege zinazotumia panga boi, haziwezi kuruka haraka kuliko sauti," anasema.

Anasema mashirika yote ya ndege yanayofanya kazi kwa sasa, kama Boeing au Airbus, yana ndege aina ya 'turbo fan au turbo jet.'

Katika teknolojia hiyo, hewa ya kasi ya juu inaachiliwa na hutolewa nje na moshi wa injini nyuma ya ndege kwa mwendo wa kasi ili kuiwezesha ndege kuruka kwa kasi kubwa.

Lakini, teknolojia inayoendeshwa na propela inafanya kazi tofauti. Inaweza kutajwa kuwa za abiria au ndege za kivita wakati wa Vita vya Pili vya Dunia vilikuwa na nguvu za propela.

"Propela inazunguka ili ndege isonge mbele. Ndiyo maana kuna ukomo wa jinsi inavyoweza kwenda kwa kasi na uwezo wake," anasema Farooq.

**KASI YA JUU**

Rolls-Royce, inasema rekodi ya awali ya ndege ya kasi ya juu zaidi inayotumia nguvu za umeme iliwekwa na Siemens mwaka wa 2017. Hata hivyo, haikuwa inatumia umeme peke yake ilikuwa na nishati mseto ya mafuta na betri na kwamba ndege yake ina umeme kamili na ina kasi ya kilomita 213 zaidi ya ndege ya Siemens.

Profesa wa vyombo vya angani katika Chuo Kikuu cha South Carolina. Tanvir Farooq anasema, "ndege za sasa zina uwezo wa kuruka kwa kasi zaidi kwa kutumia nishati ya kisukuku."

Mwendo kasi wa ndege unahesabiwa na namba ya 'mean aerodynamic chord' MAC. Hii ni namba ambayo huamua jinsi ndege inavyosafari haraka au polepole kuliko kasi ya sauti.

Kasi ya juu ya Spirit of Innovation ni MAC 0.5, ikimaanisha inaweza kwenda kwa nusu ya kasi ya sauti, lakini kasi ya kisasa ya Dreamliner Boeing-7 ni kutoka MAC 0.8 hadi 0.75 inamaana kwamba ndege hizi za kawaida zinaweza kuruka kwa kasi zaidi kuliko Spirit of Innovation.

Tanvir Farooq anasema mafanikio makubwa ya Spirit of Innovation ni kwamba inaendeshwa kwa mfumo kamili wa umeme propela ambayo inaendeshwa kwenye ndege hii inaendeshwa kwa nguvu ya betri.

Swali linabaki kuwa inawezekanaje ndege kuruka kwa kasi bila kutumia nguvu za umeme? "Kwa upande wa uhandisi na teknolojia, kumekuwa na maendeleo makubwa katika teknolojia ya betri kuanzia kipindi cha miaka minne hadi mitano iliyopita. Nguvu zake zimeongezeka sana. Ndege hiyo ni mfano wa hilo," Farooq anasema.

Anaongeza kuwa kutokana na nguvu ya juu ya betri, inaweza kuzungusha propela kwa kasi zaidi, jinsi ndege inavyokwenda mbele inategemea kasi ya propela inavyozunguka."

**BETRI NI MZIGO**

Betri inayotumika katika ndege ya Spirit of Innovation ina nguvu ya Kilo Watt (KW) 400. Wakati wa safari ya majaribio ya Spirit of Innovation, hapakuwa na abiria ila rubani. Lakini je, inawezekana kwa ndege inayotumia betri yenye mamia ya abiria kuruka kwa kasi kama ndege ya kawaida?

Wanasayansi wanasema kupaa kwa ndege kunategemea mzigo wake." Sehemu kubwa ya uzito wa Spirit of Innovation ni uzito wa betri zake. Lakini uzito wa mafuta ya ndege ya kawaida hupungua kadri inavyoendelea na safari. Lakini kwa ndege hii uzito unabaki vilevile. Kwa sababu inalazimika kubeba betri mwanzo hadi mwisho wa safari."

**BBCSWAHILI**

# Mikopo kwa wanawake na vijana, pasipo kinababa inakwamisha elimu

**INATOKA UK. 11**

huko vijijini ikilinganishwa na vijana hivyo wakipewa mikopo itawawezesha kujishughulisha na bidhaa za ngozi na kuongeza uzalishaji akitaka wakumbukwe.

"Huku vijijini sisi wakubwa ndiyo tunamiliki mifugo na ndiyo tumewagawia vijana wetu baadhi ya wanyama. Linapokuja suala la mikopo wanawalenga wanawake na vijana licha ya kwamba tuna vijana wako shuleni tunawasomesha sisi baba zao wanatutegemea, tukiwezeshwa mikopo itatusaidia kufanya biashara ya ng'ombe na ngozi na tutawainua zaidi," anasema Marwa.

Lucy Chacha, anaunga mkono suala la mikopo kutazamwa upya akisema inavyotolewa kwa kigezo cha kujiunga na vikundi imekuwa ikikwamisha ndoto za wajasiriamali wadogo kutokana na ukweli kwamba vikundi vingi hufa na kushindwa kurejesha.

"Hata hii mikopo inayotolewa na halmashauri ni changamoto ili upate mkopo mpaka lazima uwe na kikundi mkishachukua fedha baadhi ya wanakikundi wananufaika nazo wenyewe badala ya kikundi hali hiyo inasababisha mgogoro na wengine kuacha kikundi.

"Mikopo hii itolewe na kwa mtu mmoja mmoja mtu anayetamani kukopa, lakini kwa kuwa ni mikopo wa kikundi anaacha maana hanufaiki ila akiwezeshwa mwenyewe anajua atawajibika mwenyewe, lakini akiwa kwenye kundi anategemea marejesho akijua asipotoa kikundi kitawajibika." Anaeleza.

Lucy anasema ili kupunguza umaskini wa kipato vijijini ni vyema serikali ikatoa mikopo ya halmashauri kwa mtu mmoja mmoja wakiwamo wanaume, vijana, wanawake na wenye ulemavu kulingana na hitaji lake kwa kufanya hivyo itawasaidia wananchi kufanikisha malengo wanayojiwekea katika kukuza kibiashara na kuboresha maisha yao." Godfrey Chasama ni Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) - Kanda ya Ziwa iliyoko Mabuki wilayani Misungwi mkoani Mwanza, anasema sera ya nchi inaelekeza ngozi zisindikwe ndani ya nchi kwa kuwa inapochakatwa ndani ya nchi inatoa fursa ya ajira, inapandisha thamani ya ngozi ghafi na inashusha uagizwaji wa bidhaa zake kutoka nje na vyote vina matokeo chanya.

Anasema kuwa bidhaa za viatu vya ngozi vinavyozalishwa nchini vimewawezesha baadhi ya wajasiriamali wa bidhaa za ngozi kujiinua kiuchumi kutokana na kuuza bidhaa, lakini uwepo wa wajasiriamali hao unakuwa ni kichocheo cha kuongeza ubora wa kuzalisha ngozi ghafi kwani wanalipa bei ya kuvutia kwa ngozi zilizo bora.

Chasama anasema kuwa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ilitoa Sh. milioni 90 kwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na TALIRI-Kanda ya Ziwa zikishirikiana na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kutekeleza mradi yakiwamo mafunzo ya uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi ili kuendeleza mnyororo wa thamani wa mazao ya ngozi Wilaya ya Maswa mkoani wa Simiyu. Anasema kuwa katika utafiti wao bidhaa za ngozi zimeonekana kupendwa na wateja kwa kuwa ni imara na zinadumu kwa muda mrefu na zina faida.

"Tulifanya utafiti kwa wajasiriamali na vikundi vinavyojishughulisha na biashara ya viatu vya ngozi wilayani Maswa, kwa kweli ukizingatia na kwamba ndio walikuwa wanaanza walipata faida. Kwa wastani akiuza kiatu cha Sh.30,000 kati ya fedha hizo Sh.14,000 ni gharama alizotumia na Sh. 16,000 ni faida kwa kila jozi. "Labda tatizo lililopo baadhi ya wafanyabiashara wa viatu vya ngozi wanataka akianzisha biashara kwa muda mfupi apate faida kubwa papo hapo. Kila kitu kinaenda hatua kwa hatua huwezi kujilinganisha na mtu aliyefanya kazi ya viatu kwa miaka 10, huyo anakuwa ameimarika kibiashara." anasema.

Akizungumzia suala la mikopo mtafiti huyo anasema, ukitaka kumpa mtu mkopo wa kununua mashine ya kisasa inabidi uangalie, je, alipokuwa anatumia vitendea kazi vya kizamani alifika navyo wapi katika biashara hiyo? Hii ni muhimu kwani inasaidia kubaini wenye nia. Hata hivyo, hatuwezi kusema sana kuhusu hilo kwa kuwa hatutoi mikopo. Kazi yetu ni kufanya utafiti wa teknolojia zilizopo na kuziboresha ili zitumike vyema hata kama wana elimu ya kawaida na ya msingi," anasema Chasama.

Kuhusu changamoto ya utoaji mikopo kupitia vikundi Chasama anaongezea kuwa ukopaji wa vikundi ni rahisi kusaidiwa isipokuwa tatizo lipo kwa baadhi ya watu kugeuza mikopo ya vikundi kuwa ya maslahi yao binafsi.

"Vikundi vinasaidia ukitaka kitu ni rahisi kupata, lakini wakati mwingine mkopo wa mtu mmoja mmoja ni bora zaidi maana unamwajibisha moja kwa moja. Pia ni rahisi kumthibitisha na unamwezesha kujiinua na nirahisi kulipa kwa kuwa anajua ni mkopo wake mwenyewe si wa wanakikundi.

ELIMU
NA SABATO KASIKA


Mwenyekiti wa CEGODETA, Thomas Ngawaiya (kushoto) na Katibu Mkuu wa taasisi hiyo, Hamad Thao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Hoja namna wazazi watoto watakavyorudi darasani

## ▪Ushauri nasaha, mwongozo muhimu
## ▪Zitajwe huduma kabla, baada ya uzazi

UAMUZI wa serikali wa kutoa waraka namba 2 wa kuruhusu wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba, kurudi shuleni katika mfumo rasmi, unaotangazwa karibuni unaibua mjadala miongoni mwa wadau wa elimu wakidai kuna uwezekano wa baadhi ya wanufaika kujinyanyapaa wenyewe au kufanyiwa hivyo na walimu.

Ni kutokana na hali hiyo anahitajika mtaalamu wa saikolojia na ushauri nasaha kuwaweka katika bora wanufaika wa urejeshwaji pamoja na wanafunzi wengine wanaosoma nao, anasema Emmanuel Shayo, mtaalamu wa saikolojia kutoka Taasisi ya Bliss Wellness Services ya Dar es Salaam.

Katika mahojiano na Nipashe, anasema njia ambayo itawafanya wanafunzi watakaorudishwa shuleni ni kuwapa nasaha na faraja akitaka kuwapo watakaowaweka sawa pamoja na jamii ya wanafunzi na walimu inayowazunguka.

Anasema, hatua ya kurudisha wanafunzi hao shuleni katika mfumo rasmi, ni nzuri, lakini kuna changamoto anazoamini zinaweza kutatuliwa na wataalamu hao ili washauri.

"Kwa mfano wanafunzi waliorejeshwa wanaweza kujinyanyapaa kwa kujiona hawafai tena kuwa pamoja na wenzao shuleni, lakini walimu wanaweza kuwapuuza na kuwachukulia kama wazazi," anaonya Shayo.

Anafafanua kuwa mazingira kama hayo, yanahitaji kuwapo kwa wataalamu hao ili kuwasaidia kuchangamana tena: "Waliopata ujauzito, wanatakiwa kuchukua uamuzi wa serikali kama hatua muhimu kuwasaidia kutimiza ndoto zao kielimu, hivyo wasijinyanyapae, na walimu nao wawachukulie kama wanafunzi wao."

Mwanasaikolojia huyo anataja jambo jingine linalohitaji uzito kuwa ni kuhamasisha jamii, ili itambue matatizo yanayoambatana na mimba za utotoni na ifunzwe njia bora za kuyaepuka.

### MFUMO RASMI UNAUMIZA

Mkurugenzi wa Asasi isiyo ya kiserikali ya Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly, anasema, serikali ingeendelea na utaratibu alioutangaza awali wa kurejesha wanafunzi hao shuleni kwa mfumo usio rasmi. Kurudi kwa mfumo usio rasmi kungeepusha ukatili, unyanyapaa na dharau kutoka kwa wanafunzi wenzao shuleni.

"Ninadhani mfumo rasmi unaweza kuchochea mimba shuleni, kwani wanafunzi wengine wanaweza kudhani ni jambo la kawaida kubeba ujauzito, hivyo na hata kushiriki vitendo hivyo," anasema Rhobi.

Anasema, serikali ina nia njema ya kuwasaidia watoto wa kike kupata elimu, lakini anadhani mfumo usio rasmi ungekuwa njia nzuri ya kuwarejesha shuleni wale ambao wamewahi kupata ujauzito.

"Kimsingi mfumo usio rasmi unaweza kusaidia kuepusha unyanyapaa dhidi yao, vitendo vya ukatili na dharau, lakini kupunguza kasi ya mimba hizo kwa wanafunzi, hivyo serikali itathmini tena," anasema.

### UNAHITAJIKA MWONGOZO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kinaiomba serikali kuandaa mwongozo wa utekelezaji waraka Namba 2 wa mwaka 2021 wa kuruhusu wanafunzi kurejeshwa shuleni baada ya kujifungua.

LHRC inaamini kuwa mwongozo huo utaondoa ubaguzi, kutengwa na pia utawezesha kuhudumia watoto wao, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, anapozungumza na Nipashe.

Anaongeza kuwa pia ueleze pale mtoto wa kike anapopata ujauzito ni huduma gani shule inatakiwa kumpa na kumsaidia ili aendelee na masomo bila kuathrika na anaipongeza serikali kwa kutoa tamko lililofuatiwa na Waraka Namba 2 kuhusu wanafunzi waliocha shule kwa sababu ya ujauzito kurudi shuleni katika mfumo rasmi.

"Hii ni hatua kubwa kwa serikali, jamii na kwa wasichana ambao kwa muda mrefu wamekosa haki zao za elimu kwa sababu ya kutokuwa na mfumo wa kuwaruhusu kurudi shule katika mfumo rasmi," anasema Anna.

Sehemu ya waraka huo wenye kumbukumbu namba ED/OK/NE/W/VOL.II/39 inaelezea jinsi urejeshwaji huo wa wanafunzi shule unakavyokuwa na kuelekeza wadau wa elimu namna ya kuutekeleza.

Waraka huo unaeleza kuwa wanafunzi watakaokatiza masomo kutokana na ujauzito au utoro, wataruhusiwa kurudi shuleni ndani ya miaka miwili tangu walipokatiza masomo yao na wakuu wa shule na walimu wakuu wanatakiwa kuhakikisha wanafunzi waliokatiza masomo na kurudi shuleni, wanapata huduma za ushauri nasaha, ili kuwajenga kisaikolojia pamoja na wenzao waliopo shuleni.

Wakuu wa shule, walimu wakuu wanatakiwa kuhakikisha mwanafunzi aliyekatiza masomo anarejea mwanzoni mwa mwaka wa masomo katika darasa alilokuwa anasoma awali.

Aidha, unawataka walimu wahakikishe mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji unafanyika katika mazingira bora kwa wanafunzi wote na pia viongozi wa elimu katika ngazi zote wafuatilie na kutathmini utekelezaji wa waraka huo.

### MIPAKA YA WARAKA

Pamoja na kuruhusu kundi hilo la wanafunzi kurudi shuleni, serikali inaeleza kuwa hauwahusu wanafunzi waliofukuzwa shule kutokana na makosa ya jinai au mwenendo unaohatarisha amani shuleni.

Waraka huo ulionza kutumika wiki iliyopita Novemba 24, unawashauri wanafunzi watakaothibitika kutenda makosa hayo na kufukuzwa shule, waendelee na masomo kupitia elimu nje ya mfumo rasmi.

### WAPO WANAOUKATAA

Mjadala huo wa kuruhusu wasichana hao kurudi shuleni baada ya kujifungua haukubaliki kwa baadhi ya wadau wanaodai kwamba, mwanafunzi aliyekatisha masomo kwa sababu ya mimba akirudishwa shuleni, anaweza kusababisha mimba kuongezeka na hali hiyo kukubalika.

Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), inapingana na maamuzi hayo kwa maelezo kuwa serikali ilikuwa imeshatangaza uamuzi wa kurudisha wanafunzi wote waliokatisha masomo, lakini kwa mfumo usio rasmi na sasa wanashangaa kusikia utaratibu kubadilishwa.

Tangu kupata uhuru, serikali haijaruhusu utaratibu huo wa kurudisha shuleni wanafunzi wanaopata ujauzito, maelekezo ya awali yangeendelea, na kwamba suala la mabadiliko kama hayo lingehitaji maoni ya wananchi kwanza, kwa kuwa tangu zamani wale wanaopata mimba hutafutiwa njia nyingine ya kuendelea.

Mwenyekiti wa CEGODETA, Thomas Ngawaiya, anasema, kabla ya kuchukua hatua ya kutoa waraka wa kurejesha wanafunzi hao shuleni, serikali ingeunda tume ya kukusanya maoni ya wananchi kwanza ili isikie yale wanayosema.

"Ninasema hivyo, kwa sababu ni serikali hiyo ambayo ilikataa kwamba wanafunzi waliopata mimba wasiruhusiwe kurudi shuleni, lakini sasa imeamua kuwarudisha, hivyo ingepata ya wananchi kwanza," anasema Ngawaiya.

Anasema, jambo hilo limekuwa na utata tangu serikali ilipotoa msimamo wa kutoruhusu wanafunzi waliopata mimba kurudi shuleni, miaka mitano iliyopita, na kwamba utata huo ungemalizwa baada ya kupata maoni ya wananchi.

"CEGODETA tunaamini kwamba, wanaosimamishwa shule kwa sababu ya ujauzito, wanaweza kupata elimu kwa njia nyingine na ndivyo imekuwa ikifanyika miaka yote, siyo lazima warudi katika mfumo rasmi," anasema.

Anaeleza kuwa hakuna anayekataa mtoto wa kike asisome, bali tatizo ni mfumo unaotumika kurudisha wanafunzi hao shuleni, ambao taasisi yake inaona kwamba inaweza kuwa madhara baadaye.

"Serikali ina nia njema na sisi tuna nia njema kwa watoto wetu, ndiyo maana tunashauri kwa lengo la kuwafanya wanafunzi wazingatie masomo na kuepuka vishawishi ambavyo vinaweza kuwasababishia mimba," anasema.


Anasema, urejeshwaji huo kwa mfumo rasmi au usio rasmi, vinaweza kusababisha wanafunzi waliopo shuleni na wale watakaorejeshwa, kutokuwa makini, kwa kuamini kuwa hata wakipata mimba watakuwa na nafasi nyingine ya kurudi shuleni kuendelea na masomo.

ELIMU

NA HAPPY SEVERINE, MEATU

# Wafugaji 'mnafeli hapo'

## ■Kisa kuwakatisha watoto masomo, kuhamia kusaka malisho



Mtoto na mwanamama wakiwa kwenye nyendo za ufugaji. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MTINDO wa maisha ya kuhama kila wakati miongoni mwa wafugaji mkoani Simiyu, umekuwa ni kikwazo kinachowanyima mamia ya watoto haki ya kupata elimu licha ya serikali kugharamia huduma hiyo.

Mathalani, wilayani Meatu kuhama huko kunasababisha watoto wengi wenye umri wa kuanzia miaka mitano hadi 13 wa familia za wafugaji kushindwa kwenda shule.

Hayo yalielezwa na Mtendaji wa Kata ya Mwamanimba, Charles Manota, wakati wa mahojiano na Nipashe na kuongeza kuwa sababu kubwa zinafanya wananchi kuhama hama kila mwaka ni kusaka malisho ya mifugo na hali huwa mbaya msimu wa ukame.

Anasema ukame unaoikumba wilaya hiyo na kufanya watoto wengi kuondoka na walezi au wazazi wao na kukosa muda kwenda shule.

Anasema wananchi hao wanapohama na kwenda mikoa mingine ya Rukwa, Katavi na Morogoro kutafuta malisho, wamekuwa hawathamini na kuzingatia kuwapeleka watoto shuleni.

Anasema huwaacha watoto wao wadogo ila kuendelea elimu ya msingi, akieleza kuwa mwezi Julai, Agosti, Septemba, Oktoba hadi Novemba ndicho kipindi ambacho makundi makubwa ya wananchi wafugaji na wakulima wa wilaya hiyo hukimbia na kuhamia katika mikoa hiyo.

Analitaja moja ya maeneo ambayo watoto wadogo wameendelea kukosa haki za kusoma kuwa ni kata ya Mwamanimba ambayo mwaka 2019 hadi Novemba 2020 kaya nyingi zimehama na kuyakimbia makazi yao ili kufuata malisho ya mifugo bila kuwahamisha watoto wao.

"Unaweza ukaona kata nzima yenye vijiji vitano kaya zaidi ya 12 zimehama na watoto wao wanaolazimika kuacha shule na kwenda katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kutafuta maeneo ya kilimo na malisho bila kujali wanafunzi wanaohama nao wanakosa kuendelea kupata elimu."

Anaongeza: "Na ukiangalia kwa wastani kila kaya moja ina watu kuanzia sita, na kati ya hao wanafunzi ni wanne, hivyo kuna zaidi ya watu 100 wamehama kwa mwaka huo wa 2019 na hao wameondoka na watoto ambao ni wanafunzi wa shule za msingi," anasema Manota.

Anaongeza kuwa moja ya haki ambazo hawazipati watoto wa kaya hizo zinazohama kila mwaka ni elimu, kwani wengi wao huwafanyisha watoto hao shughuli za kilimo na ufugaji kwenye maeneo ambayo wanahamia na kupuuza suala la kuendelea na masomo.

Shule ya Msingi Mabambasi iliyoko Kata ya Mwamanimba, ni moja ya shule ambazo huathirika kila mwaka na kuhama huko kwa wananchi, ambao idadi kubwa ya wanafunzi huondoka bila ya taarifa na kuwakosesha haki ya msingi ya kupata elimu itakayowasaidia kumudu maisha yao.

Baadhi ya walimu wa shule hiyo wanasema kuwa wanafunzi ambao wanatoroka bila ya taarifa na wengi ni wa kutoka darasa la kwanza hadi la nne, na chekechea.

Kila wanapoanza kuwafuatilia hupewa taarifa kuwa familia zao zimehama kusaka malisho ya mifugo katika mikoa mingine.

Christopher Mwalyambi ni Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo anasema kuwa wazazi na walezi wengi wakiamua kuhama huwatoi taarifa kwenye uongozi wa shule wala wa kijiji na kuwachukua watoto wao bila ya kufuata utaratibu.

" Tunajua kuhama siyo jambo baya, lakini kwa mwanafunzi kuna taratibu za uhamisho, hilo wao hawafanya wanawatorosha na wakienda huko hawawapeleki shule tena kwani wengi wao wanakwenda kuishi porini," anasema Mwalimu Mwalyambi.

Aidha, anataja takwimu za mwaka mwaka 2019 kuwa shule ilitarajia watoto 21 walioandaliwa kuwa wangeingia darasa la awali 2020 waanze darasa la kwanza, lakini saba kati ya hao hawajulikani walipo.

Anasema watoto hao wanatoka kwenye familia mbili, ambapo wamepata taarifa zao kuwa wazazi wao wamehama na kwenda mkoani Morogoro kutokana na hali ya ukame iliyokuwamo mwaka jana.

"Tunajua watoto hao hawaendi kusoma tena, ndiyo mwisho wa elimu wanakosa haki yao ya msingi, tunajua wataendelea kupungua maana familia nyingi zinahama hasa kipindi hiki cha kilimo na ukame," anasema.

Emmanuel Zakayo ni mwalimu wa darasa la kwanza shuleni hapo, anasema mtindo huo wa kuhama unaathiri maendeleo ya taaluma kishule, kwani baadhi ya wanafunzi wanaoachishwa masomo wamekuwa na uwezo mkubwa darasani.

"Jambo hili linatuvunja moyo wa kufundisha, wanafunzi wengine unakuta wana uwezo mkubwa na mzuri darasani, lakini wanapelekwa uhamisoni na wazazi na walezi na hawapelekwi shule tena," anasema Mwalimu Zakayo.

Baadhi ya wakazi wa mji wa Mwanhuzi wanasema wilaya hiyo hapo awali ilikuwa na changamoto ya ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa hadi kupelekea kuwa wilaya ya pili kutoka mkoani mara kwa mara lakini kwa sasa tatizo hilo limeisha na changamoto mpya iliyoibuka ni wazazi na walezi kuwakatisha masomo wanafunzi kisa kuhama na mifugo.

Reuben George mkazi wa Mwahnuzi anasema serikali na wadau wa elimu waone namna ya kulitatua tatizo hilo kwa kuwajengea hosteli na mabweni ambayo yatawatunza watoto wa wafugaji na wakulima na kubaki shule kuendelea na masomo hata walezi na wazazi wao wanapotaka kuhama, anasema George.







## World Vision yaendeleza elimu kilimo chenye tija

**Na Renatha Msungu,** CHEMBA

SHIRIKA la World Vision linaendelea kutoa elimu ya kitaalamu kwenye sekta kilimo kwa wakazi wa vijiji mbalimbali mkoani Dodoma, ili kuhakikisha wanalima kilimo chenye tija.

Ofisa Mradi kutoka Shirika hilo kwa kushirikiana na maofisa kilimo kutoka serikalini wametoa elimu hiyo kwa wakulima wa Kata ya Sanzawa wilayani Chemba mkoani Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Ofisa Kilimo wa Kata ya Sanzawa, Salau Sumayi, alisema wamekuwa wakitoa elimu ya namna ya upandaji mbegu pamoja na kuwapa mbegu bora za mazao ya chakula ili kupata mavuno mengi.

"World Vision inatusaidia sana kuwainua wakulima hawa vijijini, awali wamekuwa wakilima eneo kubwa, lakini mavuno machache kwa sababu hawalimi kitaalamu," alisema Sumayi.

Alisema baada ya elimu wakulima hao hivi sasa wamevuna mazao mengi ya vyakula katika maeneo hayo.

Alisema wakulima wengi wa kata hiyo hivi sasa wanavuna mazao mengi ya chakula kutokana na kilimo cha kitaalamu ambacho wanafanya.

Alifafanua kuwa wakulima wengi hivi sasa wamekuwa wataalamu wa kilimo na kusaidia kuwafundisha wengine kulima kitaalamu ili nao wavune mazao mengi.

Naye mratibu wa mradi kutoka shirika hilo, Joseph Kilimba, alisema shirika hilo liko katika utekelezaji wa miradi mbalimbali mkoani Dodoma ili kuwainua kiuchumi wakazi wa mkoa huo.

Alisema moja ya miradi ambayo inatekelezwa ni pamoja na ule wa mama na mtoto, lakini kusaidia kutoa elimu ya utaalamu wa kilimo kwa jamii ili walime kilimo chenye tija.

Hata hivyo, alisema tangu waanze utekelezaji huo wakulima wengi hivi sasa wanafanya kilimo chenye tija.

Alisema wamekuwa wakitoa mbegu kwa wakulima ambazo ni bora pamoja na kuwaelekeza namna ya upandaji ili waweze kupata mavuno mengi wakati wa msimu wa mavuno.

Mkulima wa mazao ya chakula, Amina kutoka Sanzawa, aliishukuru World Vision kutokana na msaada wanaoutoa kwa wakulima ambao umechangia wao kuvuna magunia mengi.

Amina Mohamed alisema awali alikuwa akivuna gunia mbili au tatu kwa heka moja, lakini hivi sasa ameongeza ekari za kulima na mwaka jana amevuna mtama magunia 32 na mahindi gunia 12.

Alisema katika kata hiyo suala la njaa ni historia kutokana na kwamba wakazi wa eneo hilo wanachakula cha kutosha.

Hata hivyo, aliwataka wakulima kuendelea kufuata kilimo cha kitaalamu ili kuondokana na umaskini kupitia kilimo wanachofanya.

# Ndege tatu kununuliwa kudhibiti nzige nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kununua ndege zitakazotumika kukabiliana na nzige ambao wamekuwa wakiibuka mara kwa mara na kufanya uharibifu katika mashamba ya mazao mbalimbali nchini.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio katika sekta ya kilimo kwa waandishi wa habari kwa kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema, kutokana na kuibuka kwa nzige hao mara kwa mara, serikali imeona kuwa ipo haja kutenga fedha ili kununua ndege na kuimarisha sekta ya kilimo anga.

"Kuna shirika la kukabiliana na nzige ambalo makao makuu yake yapo kule nchini Ethiopia, lakini lipo shirika la kukabiliana na nzige wekundu makao makuu yake yapo kule Zambia na huku kote sisi ni wanachama na tunachangia fedha na wakati ambapo wale nzige waliibuka tuliomba ndege ambazo sisi pia tuna haki nazo," alisema Prof. Mkenda.

Alisema, pamoja na kuwa wanachama katika mashirika hayo, bado ipo haja ya taifa kuwa na ndege zake ambazo zinaweza kukabiliana na janga hilo mara tu linapo jitokeza.

"Pamoja na kuwa wanachama wa mashirika haya ya kukabiliana na nzige, lakini bado kama taifa tunatakiwa kuwa na ndege zetu kwa mfano kama janga hili lingeibuka katika mataifa mengi tusingeweza kuendelea kusubiria ndege hizo zitoke eneo fulani ndipo zije kwetu wakati nzige wanaendelea kuharibu mazao,"alisema Prof. Mkenda.

Prof. Mkenda alisema pia kutokana na majanga ya nzige ambayo yamekuwa yakijitokeza wameamua kuimarisha kitengo cha kilimo anga ambacho kilikuwepo zamani katika wizara hiyo.

"Tumeamua kurejesha kitengo hichi cha kilimo anga ambacho kilikuwepo zamani, kwani tulishawahi kuwa na maeneo hata ya kuhifadhi ndege zetu na maeneo ya kurukia,"alifafanua Prof. Mkenda

Akizungumzia mikakati ya wizara hiyo katika kukabilina na uagizaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo nje ya nchi, alisema wamejipanga kuimarisha uzalishaji wa kila zao ikiwamo alizeti kwa ajili ya mafuta ya kula.

"Tumepata mbegu bora takribani tani 2,000 za kisasa za zao la alizeti ambazo zitakwenda kutolewa kwa wakulima ili kulima kilimo mkataba na wazalishaji wa mafuta ya alizeti ili kukabilina na uhaba wa malighafi katika viwanda vya uzalishaji mafuta,"alisema.

Vilevile, alisema katika zao la chikichi wameshaandaa maeneo kwa ajili ya kulima zao hilo mkoani Kigoma ili kuwa na malighafi za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya kula.

"Mafuta yamepanda bei sana, hii ni kutokana na janga la UVIKO-19 kwani nchini mafuta ambayo tulikuwa tukiyategemea kutoka nje ni kutoka Malaysia ambako nako kutokana 'lock down' vibarua wa kuvuna chikichi hawafanyi kazi hivyo uzalishaji wa mafuta umeshuka sana hata gharama za meli zimepanda sana,"alisema Prof. Mkenda

Hata hivyo, alisema hadi sasa nguvu kazi ya kilimo nchini ni asilimia 58 kutoka asilimia 90 wakati Tanganyika inapata uhuru.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, akizungumza na viongozi wa maridhiano wa Wilaya ya Kondoa kwenye semina ya elimu elekezi iliyoambatana na uchaguzi iliyofanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Mfumo rahisi waombwa wanaushirika kukopa TADB

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuweka mfumo rahisi wa kuwawezesha wakulima walio katika vyama vya ushirika ili kunufaika na mikopo inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kumudu ushindani kwenye Soko Huru la Afrika (AFCFTA).

Katibu wa Jukwaa la Wakulima na wataalamu mbalimbali kutoka Wizara ya Kilimo, Anastazia Madeje, alisema hayo jijini hapa wakati akiwasilisha mambo yalijitokeza katika warsha ya sera za azimio la Malabo na mkutano kabambe wa maendeleo ya kilimo Afrika (CAADP PP).

Madeje, alisema wakulima wakiwezeshwa kupitia usharika wataweza kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuongeza thamani kwenye uzalishaji.

Alifafanua kuwa serikali ikiwekeza kwenye kilimo hai na hifadhi, iongeze bajeti kwa ajili ya tafiti na teknolojia ili kuongeza uzalishaji na kukuza uchumi.

"Kutengeneza jina, kuboresha ubora wa sera ya kulinda vya ndani, ukurasa 153 kipengele cha b383 programu ya kuendeleza sekta ya kilimo (ASDP 11), mkakati mdogo uandaliwe kwenye hili eneo ili kuchukua fursa za soko huru la Afrika, mfano Dodoma ina uzalishaji wa zabibu kwenye maonyesho ya hivi karibuni kampuni zinazotengeneza mvinyo zimejitokeza zaidi ya 50 huku bado mazao ya wakulima yanaharibikia shambani," alisema Madeje.

Aidha, alisema mabadiliko ya tabia nchi moja ya tishio kubwa la maendeleo endelevu kwa sababu inaathiri nyanja mbalimbali ikiwemo kilimo, afya, makazi ya uhakika na usalama wa chakula,"alisema Madeje.

Aliishauri wizara ya kilimo kurejesha masomo ya kilimo na kuangalia namna ya kutengeneza mitaala ya shule za msingi na sekodari ili kuwaandaa wanafunzi kujua namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Ripoti ya pili ya mapitio ya mwaka 2019 inaonyesha Tanzania haikufanya vizuri kwenye ahadi/azimio namba 6, yenye kukabiliana na mabadiliko tabianchi, moja ya pendekezo lililotolewa na umoja wa nchi huru za Afrika (AU) ni kuwa na kifungu cha bajeti kinachotumika kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Akipokea ripoti hiyo, Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Chakula katika Wizara ya Kilimo, Dk. Honest Kessy, alisema kama serikali wameipokea ripoti hiyo na kukiri kuwapo kwa changamoto ikiwamo ya takwimu za mchango wa wadau katika sekta ya kilimo.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kuboresha namna za upatikanaji wa mbegu na kufuata njia bora za kilimo ili kuwezesha wakulima kumudu soko huru la biashara.

Jukwaa hilo la wakulima na wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo linafadhiliwa na Shirika la ActionAid Tanzania.





# UDSM yatishia kuhamisha MCHAS kutoka Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam, kimetishia kuhamisha Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi (MCHAS) kutoka mkoani Mbeya kwenda katika mkoa mwingine endapo mkoa huo hautatenga eneo la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu inayohitajika.

Tishio hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye ni Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, wakati wa mahafali ya 51 ya chuo hicho yaliyofanyika jijini Mbeya.

Dk. Kikwete alilikataa eneo lenye ukubwa wa ekari 50 ambalo Mkoa wa Mbeya umetenga kwa ajili ya chuo hicho akisema halitoshi kwa ajili ya miundombinu ya ndaki hiyo, hivyo akautaka mkoa huo kutenga eneo lingine.

Alisema ili Ndaki hiyo iendelee kubakia mkoani Mbeya, uongozi wa mkoa huo unatakiwa kutoa eneo lenye ukubwa wakuanzia hekta 500 mpaka hekta 1,000.

Alisisitiza kuwa endapo Mkoa wa Mbeya utashindwa kutenga eneo hilo ndaki hiyo itahamishiwa katika mkoa mwingine ambao uko tayari kutoa eneo lenye ukubwa huo."Sisi hatuhitaji uwanja wa kujenga nyumba, tunataka eneo kubwa ambalo kubwa ambalo litatosha miundombinu yetu, kwahiyo hicho kiwanja wapewe wengine wenye uhitaji lakini sisi tutafutiwe eneo, Mkuu wa Mkoa ashirikiane na wabunge tupate eneo hilo," alisema Dk. Kikwete.

Alisema lengo la chuo hicho ni kujenga madarasa, nyumba za makazi kuishi wahadhiri na watumishi wasiokuwa wahadhiri, hospitali ya kufundishia wanafunzi, hosteli za wanafunzi pamoja na viwanja vya michezo mbalimbali. Alisema wanahitaji eneo ambalo litatosheleza mahitaji ya ndaki hiyo kuanzia miaka 100 ijayo huku akisisitiza kuwa eneo la kampasi kuu iliyopo mkoani Dar es Salaam, lingetolewa dogo wakati huo kwa sasa lingekuwa halitoshelezi mahitaji.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Mwanaidi Mtanda, alisema Serikali ya Mkoa wa Mbeya imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 50 lililopo Forest Mpya ndani ya Jiji la Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Ndaki hiyo. Alisema ili ndaki hiyo iendelee kustawi na kupanuka uongozi wa chuo hicho unategemea ushirikiano wa viongozi wa Mkoa wa Mbeya pamoja na wananchi akidai kuwa uwapo wa ndaki hiyo ni kwa faida pia ya wananchi wa mkoa huo.

"Chuo hiki ni miongoni mwa vyuo vikongwe katika ukanda wetu huu wa Afrika ya Mashariki, lakini mahafali haya ni ya pili kuwa ya kihistoria maana yamefanyika katika Mkoa wa Mbeya, lengo ni kuendelea kukitangaza chuo chetu kwa wananchi," alisema Mwanaidi.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, alisema chuo hicho kwa sasa kina mpango wa kufikia usawa kwenye udahili wa wanafunzi wa kike na wa kiume.

Alisema wamefikia asilimia 47 wanafunzi wa kike na 50 wa kiume na kwamba kwa mwaka ujao wanatarajia kufikia 50 kwa 50.




Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Jakaya Kikwete (mwenye kofia nyekundu), akiwaongoza washiriki wa Mahafali ya 51 ya Chuo hicho Ndaki ya Afya na Sayansi ya Jamii (MCHAS) iliyoko jijini Mbeya mwishoni mwa wiki kuimba Wimbo wa Taifa. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

## Watafiti, wanasayansi watakiwa kubuni mbinu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANASAYANSI na watafiti wa magonjwa ya binadamu nchini wametakiwa kubuni mbinu za kisayansi ambazo zitasaidia kutatua matatizo mbalimbali ya dunia, ikiwamo kusaka dawa za kutibu Virusi vya Ukimwi badala kuishia kukusanya takwimu za matatizo.

Ushauri huo ulitolewa juzi jijini Mbeya na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alipokuwa anafunga kongamano la siku mbili la kisayansi la kitaifa kuhusu Virusi vya Ukimwi ikiwa ni mwendelezo wa Maadhimisho ya Wiki ya Ukimwi duniani.

Alisema endapo wataalam hao watabuni teknolojia za kuleta suluhisho la matatizo yanayoikumba dunia kuna uwezekano uchumi wa taifa ukakua kutokana na mauzo ya teknolojia hizo nje ya nchi.

Alisema kwa sasa wataalamu wanaishia kukusanya zaidi takwimu za matatizo badala ya kutafuta suluhisho la matatizo hayo, na kwamba kutokana na tatizo hilo la wataalamu, serikali inatumia fedha nyingi kununua teknolojia nje ya nchi.

Dk. Mollel alisema kwa sasa serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni sita kwa ajili ya kuwawezesha wanasayansi wazawa kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo za kutatua matatizo ya wananchi.

"Endapo wataalamu wetu hawa watabuni teknolojia, dawa na tiba kwa ajili ya magonjwa mbalimbali, gharama za matibabu zitapungua kwa kiwango kikubwa na hata mataifa mengine tutayauzia teknolojia zetu, hivyo nimewaachia wanasayansi wetu changamoto hiyo," alisema Dk. Mollel.

Mkurugenzi wa Utafiti wa Chuo Kikuu cha Muhimbili, Prof. Bruno Sunguya, alisema katika kongamano hilo walijadili tafiti mbalimbali ambazo ziliwasilishwa na watekelezaji pamoja na wadau wa Afua mbalimbali za Ukimwi.

Alisema walijadiliana na kubainisha matatizo mbalimbali yanayowakabili wadau wakati wa utekelezaji wa afua mbalimbali za Ukimwi pamoja na kupanga mikakati ya namna ya kukabiliana na matatizo hayo.

"Kulikuwa na mada 34 ambazo zimewasilishwa hapa na zipo zingine tisa ambazo zimewasilishwa kwa njia ya posta, na kuna mambo ambayo tumejifunza kutoka kwa wenzetu wa mataifa mengine," alisema Prof. Sunguya.

Alisema kutokana na changamoto waliyopewa na Dk. Mollel watahakikisha wanashirikiana kufanya tafiti ili kuleta suluhisho la matatizo mbalimbali yanayowakabili watanzania.

# Majaliwa aikataza TRA ufungiaji wa biashara

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kuisimamia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iache kufunga biashara za wawekezaji na wajasiriamali wenye matatizo kwenye ukusanyaji wa mapato.

Aliitaka mamlaka hiyo kutatua matatizo hayo kwa njia ya mazungumzo pamoja na kukusanya kodi kistaarabu badala ya kutumia mabavu ili kuchochea ukuaji wa biashara pamoja na kuvutia wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza nchini.

Alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kikazi wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya ambako alitembelea viwanda mbalimbali vikiwamo vinavyozalisha maji, ambapo alisema utaratibu unaotumiwa na TRA unawakatisha tamaa wawekezaji.

Alisema matatizo yote yanayohusiana na masuala ya kodi yanatakiwa kutatuliwa kwa majadiliano badala ya kutumia mabavu ikiwamo kufunga biashara za watu jambo ambalo alidai ni usumbufu kwa wafanyabiashara.

"Ofisi yangu itahakikisha inaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na tayari nimeshatoa maelekezo, tunahitaji wawekezaji wetu hasa wa ndani wanafikia hatua wanakuwa wawekezaji wakubwa wenye mitaji mikubwa," alisema Majaliwa.

Alisema uwapo wa wawekezaji wengi unasaidia kupunguza umaskini nchini kwa kuongeza mzunguko wa fedha pamoja na kuongeza wigo wa ajira kwa wananchi wa Tanzania.

Baadhi ya wawekezaji wilayani Rungwe walisema tatizo kubwa linalowakabili kwenye maeneo yao ni ubovu wa miundombinu ya barabara na hivyo wakaiomba Serikali iwasaidie kuboresha miundombinu hiyo.

Msimamizi wa Kiwanda cha kuzalisha maji cha Tukuyu Spring Water, James Mgeni, alisema katika eneo la Wilaya ya Rungwe maeneo mengi miundombinu ya barabara siyo ya kuridhisha hasa zinazoingia vijijini ambako ndiko kwenye uwekezaji mkubwa.

Alisema kwa sasa bidhaa wanazozalisha ni nyingi na zina uhitaji mkubwa, lakini ubovu wa barabara unasababisha wateja kushindwa kufika kwa urahisi kwenye maeneo yao.

"Sisi ukiacha kiwanda hiki lakini pia kule Mbozi mkoani Songwe pia tunavyo viwanda ambavyo tunazalisha mafuta, tunakoboa kahawa na tunasaga nafaka na kote huko miundombinu ya barabara ni mibovu, tunaomba tusaidiwe," alisema Mgeni.

Akijibu tatizo hilo la wawekezaji, Waziri Mkuu aliwaagiza wakuu wa wilaya zote nchini kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa barabara zinazopita kwenye maeneo ya wawekezaji ili kuondoa tatizo hilo na shughuli zao zifanyike kwa urahisi. Aliwataka wakuu hao wa wilaya kusimamia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili wazijenge barabara hizo kwa viwango ambavyo vitasaidia shughuli za wawekezaji kuendelea.

Aliwataka wawekezaji wenye uwezo pia kushirikiana na Serikali kuboresha miundombinu ya barabara zinazopita kwenye maeneo yao huku akisisitiza kuwa hawatakiwi kuachiwa kazi hiyo peke yao.



## TPSF yajitosa kuhamasisha ukuzaji biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imeanzisha mradi wa Africa Franchising Accelerator (Afrap) ili kuwahamasisha wafanyabiashara kukuza biashara zao katika mfumo wa pamoja na kujulikana kimataifa.

Hayo yalielezwa juzi na mshauri mwelekezi wa Afrap, Wambugu Wa Gichohi, wakati akizungumza na waandishi wa habari Zanzibar kuhusu kazi za taasisi hiyo.

Alisema mfumo huo unatumika sehemu nyingi dunia lakini kwa Tanzania na Afrika dhana ya matumizi ya mfumo huo bado haijajulikana kwa wafanyabiashara jambo linalowafanya washindwe kukuza biashara zao.

Alisema mfanyabiashara mdogo hawezi kufikia soko kubwa, lakini anapokuwa ameunganishwa na wengine kupitia mifumo ya kisasa ya kimtandao itamiwezesha mkulima kupata soko kubwa duniani.

Alisema kuwa ukosefu wa soko la bidhaa zinazozalishwa hapa ndani na wafanyabiashara wadogo na wakati ni miongoni mwa changamoto zinazowakwamisha kukua kibiashara katika ngazi za kimataifa.

"Wafanyabiashara wengi wamekuwa wakianzisha biashara zao lakini wanashindwa kukua kwasababu ya kukosa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema kwa kushirikiana na Taasisi ya Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Zanzibar, wanaandaa mafunzo maalumu kwa ajili kuwapa elimu wafanyabiashara ili wapatikane watakoweza kujiunga katika mfumo huo wa pamoja.

"Kuna wale ambao wanaendesha biashara zao mmoja mmoja na ni wadogo tutawaunganisha kupitia vyama vyao na tutatengeneza umoja ambao utaingizwa kwenye mfumo ambao ni rahisi kulifikia soko la dunia tofauti na mtu kuwa mmoja.

Kwa upande wao wafanyabiashara Mjini Zanzibar wamefurahishwa na ujio wa taasisi hiyo ambayo inalengo la kuwainua wafanyabiashara.

Ali Issa alisema hivi sasa biashara ni ngumu kutokana na janga la corona, hivyo taasisi hiyo imekuja muda mwafaka.

# Sababu wagonjwa wa akili waliokimbia kurudi hospitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UWAPO wa jengo jipya la hospitali ya wagonjwa wa akili Zanzibar umesaidia kuwarejesha baadhi ya wagonjwa waliokimbia kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Akizungumza na Nipashe daktari bingwa wa magonjwa ya akili hospitalini hapo, Khadija Abdulrahman Omar, alisema awali wagonjwa hao walikuwa wakilazwa katika jengo moja la zamani ambalo limechakaa hivyo baadhi ya wagonjwa walikimbia hawapataki lakini sasa wameanza kurejea.

Alisema awali ilikuwa ni ngumu kuwahudumia wagonjwa kutokana na wagonjwa hao kuwepo sehemu moja ambapo baadhi ya wagonjwa huwa wakali huwashambulia wafanyakazi na wagonjwa wengine.

"Wagonjwa wengine wanapigana inakuwa vigumu kuwadhibiti kutokana na upungufu wa dawa...baadhi ya wafanyakazi wameshatafunwa masikio na wagonjwa wale ambao huwa wakali...lakini katika jengo jipya ni rahisi kuwadhibiti tunajihisi kama tupo ulaya katika jengo hili jipya," alisema.

Alisema kuwa uwepo wa jengo hilo wananchi wanaofuata huduma hospitalini hapo wamefurahi na uwepo wa jengo hilo litaondoa hali ya unyanyapaa kwa wagonjwa wa akili kutokana na mwonekano wa awali wa jengo la zamani hospitalini hapo.

"Jengo hili la kisasa ni la kipekee na litaondoa hali ya unyanyapaa kwa jamii ambapo hospitali yetu ya wagonjwa wa akili wanaliita jela ya wendawazimu kutokana na jengo hilo limechakaa na la zamani,"alisema Khadija ambaye ni daktari wa dhamana wa hospitalini hapo.

Alisema jengo hilo jipya lina wodi la kulaza watu wazima wenye magonjwa ya akili, jengo la kuzala watoto wenye tatizo la afya ya akili na jengo la uraibu ambao wanatumia dawa za kulevya.

Alisema hata jamaa wa wagonjwa wamefurahi kuona kuwa wagonjwa wao wanahudumiwa katika mazingira yanayovutia na salama zaidi kwa ajili yao ili kusaidia kurejesha hali zao za afya ya akili.

Alisema kuwa bado kuna unyanyapaa kwa wagonjwa wa akili katika jamii na baadhi ya wazazi wanaowafikisha wagonjwa wao hospitalini hapo huwatelekeza.

"Unyanyapaa bado upo, mtu akiugua ugonjwa wa akili anaonekana hawezi kufanya jambo lolote katika jamii na hata uhudumikiaji wao ni tofauti wanatuachia wagonjwa hapa hawawapitii mpaka tunawapelekea majumbani mwao wanapopona na kuruhusiwa kutoka hospitali," alisema.

Alisema ugonjwa wa akili ni sawa na magonjwa mengine, hivyo si vyema kuwakimbia wagonjwa na ugonjwa huo hauchagui unaweza kumpata mtu yoyote.

Alieleza kuwa kuna ongezeko kubwa la wagonjwa wa akili ambao ni wanaume kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Naye Suleiman Abuu Ali Mratibu wa Afya ya Akili Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, alisema kuwa hivi sasa idadi ya watu wanaofata huduma hospitalini hapo imeongezeka na wastani kwa mwezi wanapata wagonjwa wapya 300.

Jengo hilo jipya la wagonjwa wa akili lilizinduliwa mwanzoni mwa mwezi huu na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambapo Serikali ya Norway imesaidia ujenzi huo.




Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Beatrice Mutayoba, akizungumza kwenye uzinduzi wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi aliwahamasisha wananchi kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa Uviko-19 jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# 'Watu wenye ulemavu wana haki sawa na watu wengine'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IMEELEZWA kuwa watu wenye ulemavu wana haki ya kushirikishwa katika nyanja zote za kiuchumi kama raia wengine wote bila ya kujali ulemavu wao.

Baraza la Watu wenye ulemavu Zanzibar limesema kwamba kinachoangaliwa si ulemavu wao bali ni haki zao na uwezo walionao.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Salma Saadat Haji, aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu ambayo huadhimishwa kila ifikapo Desemba 3, ya kila mwaka.

Mwenyekiti huyo alisema haki ya kushiriki katika harakati za maendeleo imeelezwa kwenye Ibara ya 29 ya Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu ulioridhiwa na Tanzania mwaka 2009.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeweka mwongozo maalum ili maendeleo ya nchi yasiwaache nyuma watu wenye ulemavu kwa kuboresha muundo wa taasisi ya watu wenye ulemavu.

Alisema maboresho hayo ni pamoja na kuanzisha maofisa wenye ulemavu mikoa, wilaya na kamati za shehia jambo linalorahisisha kuibua changamoto mbalimbali za watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya shehia na serikali kuzifanyia kazi kwa haraka changamoto hizo.

Naye Mkurugenzi Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, Mhandisi Ussy Khamis Debe, alisema kuna mafanikio mengi yaliyopatikana tokea ilipokuwa idara hadi baraza ikiwamo kuwa na takwimu za watu wenye ulemavu kupitia usajili na mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama mfumo jumuishi

Injinia Ussy alisema kuwapo kwa mpango mkakati wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu (2019 - 2024) utasaidia baraza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuishauri serikali hatimaye kutekeleza vyema masuala muhimu ya watu wenye ulemavu

Kauli mbiu ya mwaka huu katika maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu inasema "Uongozi na Ushirikishwaji Watu wenye Ulemavu, kuelekea Ujumuishwaji na Ufikiwaji endelevu baada ya UVIKO-19 duniani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MASUMBUKO JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0131-0029** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAZENGO SEKONDARI mwaka 1988. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No: 991083097266.**

116593002

## KUPOTEA KWA CHETI



**PAUL GAMBA MWIRA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.4340/0074** kilichotolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia **GIRANGO SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAR/BS/RB/120014/2021.**

116593102

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.144/ 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOSEPH EMANUEL KIMOLO Of MAKOLE Area within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CONSTANCE JOSEPH MGANGA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of PROBATE Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 3/12/2021

Date at Dodoma this 12 Day of October,2021

RESIDENT MAGISTRATE

116592902

**CHANGE OF NAMES**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT/CAP 117 2019**

**DEEDPOLL OF CHANGE OF NAME**



**BY THIS DEED I, leornard Hagai Maleko** of p o box 20360 dar es salaam, **DO HEREBY** absolutely renounce and abandon the use of my former names of **leonard Gay Maleko.** **AND IN PURSUANCE** of such changes of names as aforesaid, **I HEREBY DECLAR**E that I shall at all times hereafter and all records,deed and instruments in writing and in all actions,proceedings,dealings,transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said names **Leonard Hagai Maleko** herein above renounceand abonden.

**AND I HEREBY AUTHORISED AND REQUEST** all persons to designate and address me in the name of leonard Hagai Maleko

**THE REASON FOR THE CHANGES** IS there was a mistake on the name **Gay instead of Hagai**

**IN WITNESS WHEREOF,I** have hereto set my hand at dar es salaam this 26th day of October in the year of our Lord 2021.

116592202

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 62 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late ALEX MALIMI**

**BY 1. AGNES PAUL**
**2. .......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 13 day of 12....2021

Dated at Morogoro this 29 day of 11.....2021

RESIDENT MAGISTRATE

116593402

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 56 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late MIRAJI KIMALI KATULAGAZA**

**BY 1. CHARLOTTE SALVATORY NJOVU**
**2. .......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 7 day of DECEMBER....2021

Dated at Morogoro this 23 day of NOVEMBER.....2021

RESIDENT MAGISTRATE

116592602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATUS BALIFIKI GWAHO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 975 DJM – TOYOTA HARRIER.** Chassis namba **ACU300004121.** Engine namba **2AZ1122561.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/472817/2021.**

111659002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA2**

**Katika mahakama ya mwanzo ARUSHA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 428/2021**

**Ombi la NASOLWA NITWA KULYAMA kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu JOYCE NASOLWA SHUNU kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 7/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Wosia ya marehemu huyo upo mahakama waweza kukaguliwa

116592702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA/63) (MADAI YA TALAKA)**

**Mahakama ya mwanzo ya ....Hale.....Wilaya ....Korogwe**
**MADAI NAMBARI........4.............YA...2021**

**Mdai.......Rodgers Samweli Mdoe......**

**Mdaiwa.......Veronica Paulo Msengi.........**

**Kwa.......Veronica Paulo Msengi wa Magu Mwanza**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba anakudai wewe talaka/kuachana**

Kwa hiyo unawajibika wewe binafsi kuhudhuria katika Mahakama hii ya siku ya Ijumaa 26-11-2021 saa 2:00 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri, ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazokuhusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikidhibitika kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii.

Hakimu Mahakama ya Mwanzo

116592802

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Afrika Kusini yaalani katazo safari za ndege nchini mwake

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa, amelaani hatua ya mataifa mbalimbali duniani, kuamua kusitisha safari za ndege kutoka nchini mwake na nchi jirani, baada ya kugundulika kwa kirusi kipya cha COVID-19 kilichopewa jina Omicron, wiki iliyopita.

Ramaphosa amesema amesikitishwa na hatua ya mataifa hayo, ambayo ni pamoja na Marekani, yale ya Umoja wa Ulaya (EUO na Uingereza, na kusisitiza kuwa kitendo hicho hakikustahili kufanyika na kutaka uamuzi huo kubadilishwa haraka iwezekanavyo.

**Mpaka sasa kirusi hicho cha Omicron, kimeripotiwa nchini Uingereza, Ujerumani, Australia na Israeli.**

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema, kirusi hicho kipya ndio chanzo cha kusambaa kwa maambukizi makubwa katika Mkoa wa Gauteng, nchini Afrika Kusini kwa kipindi cha wiki mbili zilizopita.

Hata hivyo WHO nayo inaonya dhidi ya uamuzi wa mataifa mbalimbali kuzuia safarai za ndege na kuchukua hatua nyingine, kwa kile inachosema hatua za kisayansi ndizo zinazopaswa kuchukuliwa.

Aidha, watalaamu wa shirika hilo la afya, walisema itachukua wiki kadhaa kubaini undani ya kirusi hiki ambacho kimezua wasiwasi duniani.

Mpaka sasa kirusi hicho cha Omicron, kimeripotiwa nchini Uingereza, Ujerumani, Australia na Israeli, ambayo imetanagaza kufunga mipaka yake. **RFI**



Wapitanjia wakikatiza kwenye barabara iliyozuiwa na waandamanaji kwa kuchoma moto matairi kutokana na kupinga kudorora kwa hali ya uchumi, mjini Beirut, nchini Lebanon, jana. **PICHA: REUTERS**

## Mahakama Botswana yaidhinisha kutobaguliwa wapenzi jinsi moja

**Gaborone,** BOTSWANA

MAHAKAMA ya Rufani ya Botswana, imeidhinisha uamuzi wa mwaka 2019 wa kutowabagua wapenzi wa jinsi moja.

Majaji watano wa mahakama hiyo, waliidhinisha kwa kauli moja kwamba kuwabagua watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsi moja, kulikiuka haki za kikatiba za wapenzi wa jinsi moja wa kike, wakiume, wenye jinsi mbili na waliobadili jinsi zao, (LGBT)

Mwaka 2019, mahakama ya juu ilipinga kuwa sheria zilizoweka zinazoidhinisha hadi kifungo cha miaka saba kwa wanaoshiriki mapenzi ya jinsi moja, ikizitaja kuwa kinyume cha Katiba,

Imesema pia kuwa utu wa binadamu unadhurika wakati makundi ya raia walio wachache yanapoachwa nyuma.

Taifa lilikata rufaa dhidi ya uamuzi huo, likidai kanuni ya adhabu ni zaidi ya ngono ya wapenzi wa jinsi moja. Ilisema pia kwamba raia walio wengi hawakuafiki uamuazi wa mwaka 2019.

Uamuzi wa Jumatatu unaondoa vipengele viwili vya sheria ya adhabu vilivyokiuka sheria kuhus mapenzi ya jinsi moja.

"Vipengele hivyo viliondoa maana yake na kuegemea utashi wa idara za utekelezi wa sheria na hivyo kuwafanya wawe watu wa kuingilia maisha ya binafsi ya raia ," alisema Jaji wa mahakama ya rufaa, Ian Kirby, aliyeongoza mchakato wa utoaji wa hukumu hiyo.

Sheria zinazopinga mahusiano ya kingono ya watu wa jinsia moja zipo katika nchi nyingi kati ya nchi 54 za Afrika. **BBC**

## Ethiopia imekanusha shambulizi

**Khartoum,** SUDAN

JESHI la Sudan limesema Jumapili kwamba wanajeshi wake sita, wameuawa wakati wa mapambano kwenye mpaka na Ethiopia.

Tukio hilo limefanyika siku moja baada ya madai kwamba wanajeshi wa Ethiopia pamoja na wapiganaji walifanya mashambulizi kwenye eneo la mpaka, ambalo limekuwa likizozaniwa kwa muda mrefu la Al Fashaqa.

Ripoti iliyotolewa na chombo cha habari cha serikali mwishoni mwa wiki, ilisema kwamba wanajeshi wamepelekwa kwenye eneo hilo, ili kuwalinda wakulima wanaovuna vyakula vyao.

Hayo yanajiri wakati Sudan ikikabiliwa na misukosuko baada ya wakuu wa jeshi kuipindua serikali ya mpito ya kiraia mwishoni mwa Oktoba, huku zaidi ya maafisa 100 wakiwa wamekamatwa.

Maandamano makali yalifuatia hatua hiyo na kupelekea kundi hilo kumrejesha tena madarakani waziri mkuu Abdalla Hamdok.

Hata hivyo makundi yanayodai demokrasia, yanaendelea kuushinikiza utawala huo kuwaachilia maofisa waliozuiliwa, pamoja na kuruhusu utawala wa kiraia.

Ethiopia, imekanusha kufanya shambulizi mwishoni mwa juma katika eneo la mpaka wake na Sudan, ikitaja machafuko yanayotokana na uasi wa eneo lenye mzozo wa Tigray kuwa sababu.

Katika taarifa iliyotolewa na vyombo vya habari vya umma, Msemaji wa Serikali Ethiopia, Legessa Tulu ameyakanusha madai hayo na kwa kulinyooshea kidole kwa kundi la harakati la Tigray People's Liberation Front (TPLF).

Jumamosi jeshi la Sudan lilisema wanajeshi kadhaa wameuawa katika shambulizi lililofanywa na makundi yenye kujihami kwa silaha, ambayo yana uhusiano na jeshi la Ethiopia katika eneo la Al-Fashaqa.

Eneo hilo limekuwa chanzo cha mvutano kati ya serikali za Addis Ababa na Khartoum kwa muda mrefu, mwaka uliopita, pia kulizuka mapigano ambayo yalisababisha mauaji. **DW**

## Wayahudi 3,000 wa Ethiopia kuhamia Israel

**Jerusalemu,** ISRAEL

SERIKALI ya Israel imeidhinisha uhamiaji wa maelfu ya Wayahudi kutoka Ethiopia, inayokumbwa na vita, ambao baadhi yao wamesubiri kwa miongo kadhaa kuungana na jamaa zao nchini Israel.

Uamuzi huo ulichukua hatua kuelekea kusuluhisha suala ambalo kwa muda mrefu limetatiza uhusiano wa serikali na jamii ya Ethiopia nchini humo.

Wayahudi wa Ethiopia wapatao 140,000 wanaishi Israeli. Viongozi wa jamii wanakadiria kuwa takriban wengine 6,000 wamesalia nyuma nchini Ethiopia.

Ingawa familia hizo ni za asili ya Kiyahudi na wengi wao ni Wayahudi, Israeli haiwaoni kuwa Wayahudi chini ya sheria za kidini.

Badala yake, wamekuwa wakipigania kuingia nchini, chini ya mpango wa kuunganisha familia, ambao unahitaji idhini maalumu ya serikali.

Wanaharakati wa jamii wameishutumu serikali kwa kujikokota katika kutekeleza uamuzi wa 2015 wa kuwaleta Waethiopia wote waliosalia wa ukoo wa Kiyahudi nchini Israeli ndani ya miaka mitano. **BBC**

HABARI MICHEZO

# KIRENGO, WANAMAJI KUVAANA J'PILI FAINALI UMOJA CUP 2021

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Umoja Cup (ABEGA), Shirati Mji FC, wameaga michuano hiyo baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Wanamaji FC, kwenye mechi kali ya nusu fainali iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Maji Sota wilayani Rorya.

Kwa matokeo hayo, sasa Wanamaji FC watakuwa na shughuli pevu Jumapili wiki hii kwenye mechi ya fainali watakaposhuka dimbani kuvaana na Kirengo FC ambayo Jumamosi iliyopita nayo ilipata ushindi kama huo dhidi ya Mennonite FC kwenye nusu fainali ya kwanza iliyopigwa uwanjani hapo.

Pamoja na ushindi huo kwa Wanamaji FC, pia wamelipa kisasi cha kutolewa na Shirati Mji katika hatua hiyo ya nusu fainali mwaka jana.

Alikuwa ni Zeki Uromi, aliyeizamisha Shirati Mji mapema tu katika dakika ya tisa, kwa shuti kali kutoka umbali wa takriban mita 28, bao ambalo lilidumu kwa dakika zote 90 za mchezo huo uliohudhuriwa na mashabiki wengi.

Katika mchezo huo, Shirati Mji, ilicheza pungufu baada ya nahodha wao, Omega Mwasi, kutolewa nje kwa kadi nyekundu kutokana na kuonyesha utovu wa nidhamu kipindi cha kwanza kwa kutoa lugha zisizo na staha kwa mwamuzi.

Licha ya kutolewa nje, Omega aliendelea kuonyesha utovu wa nidhamu wakati timu zikijiandaa kwenda mapumziko baada ya chukua mpira na kisha kumbabua nao mwamuzi wa mchezo huo, Nasibu.

Kwa kadi hiyo nyekundu, sasa Omega atakosa mchezo wa kutafuta mshindi wa tatu kati ya Shirati Mji na Mennonite unaotarajiwa kupigwa Uwanja wa Maji Sota Ijumaa wiki hii.

Akizungumzia utovu huo wa nidhamu ulioonyeshwa na Omega, Katibu wa Kamati ya Maadili ya Umoja Cup, Telly Micky, amesema kamati yake itakaa kesho, Jumatano kujadili matukio mawili yaliyojitokeza katika nusu fainali ya kwanza ambapo mashabiki walifanyiana fujo mpaka polisi kuingilia kati na kitendo kilichoonyeshwa na nahodha huyo wa Shirati Mji katika nusu fainali ya pili.

Katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza iliyopigwa Jumamosi, Anthony Nichola, ndiye aliifungashia virago Mennonite FC baada ya kuifungia Kirengo FC bao pekee dakika ya 64 lililodumu hadi mwisho wa mchezo.

Pamoja na mvua kubwa kunyesha, mchezo huo ulikuwa kivutio kutokana na ushindani mkali na ilimlazimu mwamuzi Francis Azaria Kembo kuusimamisha kwa dakika 20 baada ya mashabiki wa Mennonite kuanzisha vurugu dhidi ya mashabiki wa Kirengo waliokuwa washangilia bao hilo, hata hivyo vurugu hizo zilizimwa na askari waliokuwapo uwanjani hapo kuhakikisha usalama unakuwapo.

Michuano hiyo ya Umoja Cup, imekuwa ikidhaminiwa kwa mwaka wa tisa sasa na mdau kubwa wa soka wa Rorya, Peter Owino.




Kikosi cha Kirengo FC ambacho Jumapili wiki hii kitavaana na Wanamaji FC kwenye mechi ya fainali ya Umoja CUP 2021 itakayopigwa Uwanja wa Maji Sota, Rorya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachezaji TBS wajivunia mafanikio SHIMMUTA

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

WACHEZAJI wa Timu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wamejivunia mafanikio makubwa ambayo timu za shirika hilo zimepata kwenye michezo ya Shirikisho la Mashindano ya Mashirika Umma na Binafsi (SHIMMUTA) yaliyomalizika mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro.

Akizunguza na waandishi wa habari juzi mkoani Morogoro, Katibu wa Michezo wa TBS, Nyabuchwenza Methusela, alisema pamoja na wachezaji wake kushiriki mashindano hayo, imekuwa fursa nzuri kwao kuwa pamoja na wenzao wa mashirika mengine.

Alisema wao kama TBS wameshiriki michuano ya SHIMMUTA ambayo imeshirikisha mashirika ya umma, binafsi na wamepata manufaa mengi, ikiwamo kuwaweka pamoja, kujenga urafiki, kufahamiana, lakini kutangaza mashirika yao.

"Kuna mashirika mengi ya umma na binafsi hapa nchini, lakini wakati mwingine kuyafahamu inakuwa vigumu, ila kupitia michezo tunafahamiana na mashirika hayo ikiwa ni pamoja na kujua yanajishughulisha na nini," alisema Methusela.

Katika mchezo wa pete wanawake timu ya TBS iliibwaga Timu ya Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa mabao 38-28, wakaitandika Benki Kuu Tanzania (BoT) kwa mabao 52-12 na kisha kuibuka na ushindi wa mabao 40-12 dhidi ya Mwalimu Nyerere.

Ushindi mwingine kwenye mchezo huo ambao timu hiyo ilipata ni wa mabao 28-15 dhidi ya Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU)

Kwa upande wa soka, TBS ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), ikapata ushindi mwingine wa mabao 2-0 dhidi ya timu ya Mkemia Mkuu, huku kwenye mpira wa wavu ikipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya TANAPA.

Timu hiyo pia ilipata ushindi mwingine katika mpira wa miguu wa mabao 4-0 dhidi ya Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA) na kisha kuitandika timu ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) 4-0.

Mashindano ya SHIMMUTA ambayo mwaka huu yalishirikisha taasisi za umma na za binafsi 41, yalianza Novemba 13, mwaka huu na kumalizika Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

# Tembo Warriors, Karafuu Empire zapigwa CANAF

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Walemavu 'Tembo Warriors', imepoteza mechi yao ya pili kwenye michuano ya Afrika (CANAF), baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Uganda, kwenye mchezo wa hatua ya makundi uliopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam jana huku ndugu zao wa Zanzibar 'Karafuu Empire' wakilala kwa mabao 5-0 dhidi ya Kenya.

Tembo Warriors ilianza vema kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Morocco wakati wenzao Karafuu Empire walianza kwa kichapo cha mabao 12-0 dhidi ya Angola, kabla ya jana wawakilishi hao wa Tanzania wote kuangukia pua dhidi ya Uganda na Kenya.

Katika mchezo wa jana kati ya Tembo Warriors na Uganda, ulikuwa na ushindani mkali, lakini hadi dakika 50 mechi hiyo zinamalizika timu hiyo ya Tanzania Bara ilitoka kichwa chini kwa bao pekee hilo lililofungwa dakika ya 20 na Ssempija Julius.

Tembo Warriors itashuka tena dimbani leo dhidi ya Siera Lione katika mchezo wao tatu, na timu zote zinahitaji ushindi katika mchezo huo hasa Tanzania ili kusonga mbele.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Tembo Warriors, Salvatory Edward, alisema wachezaji wake hawakuwa makini na wapinzani wao walitumia mapungufu yao kuwaadhibu.

Alisema kwa sasa wanasahau matokeo hayo na kuyachukulia kama funzo kwao kujiandaa kwa mechi ya leo ambayo itatoa maamuzi ya kusonga mbele ama la.

"Ukiangalia katika kundi letu timu zote zina pointi sawa kila mmoja ana alama tatu, Morocco wanaongoza kwa sababu wana bao moja zaidi, na sisi hatua bao, hivyo tunalazimika kupambana kutafuta matokeo dhidi ya Sierra Leon," alisema Salvatory.

Alisema ni mechi muhimu sana kwao kuongeza umakini na kutafuta ushindi dhidi ya Sierra Leon, kwa sababu kundi lao kila mmoja ana nafasi ya kusonga mbele na hiyo inategemea na matokeo ya mechi ya wapinzani wao.

Mbali na mechi ya Tanzania dhidi ya Sierra Leon, mchezo wa pili utakuwa kati ya Morocco na Uganda katika kundi lao hilo la AA.

Matokeo mengine ya mechi iliyochezwa jana, Morocco iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Sierra Leon.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MODRIC KUTUA UNITED
KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Luka Modric mwenye umri wa miaka 36, yuko tayari kuungana na Manchester City atakapokuwa mchezaji huru majira yajayo ya joto. **(SuperDeporte)**

### GRILLITSCH AGOMBEWA
NEWCASTLE wako kwenye kinyang'anyiro na AS Roma cha kuwania saini ya kiungo wa kati wa Hoffenheim, Florian Grillitsch mwenye umri wa miaka 26 Januari. **(Sun)**

### KAMARA AGEUKA LULU
BAYERN Munich na Barcelona kwa pamoja wanamtaka mlinzi wa Ufaransa, Boubacar Kamara mwenye umri wa miaka 22, anayechezea klabu ya Marseille. **(Footmercato's Santi Aouna on Twitter)**

### DEMBELE AIKATALIA BARCA
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Ousamane Dembele amekataa ofa ya kuongezewa mkataba na Barcelona wakati huu nyota huyo mwenye miaka 24 akikaribia kuwa mchezaji huru. **(Sport)**

### FULGINI ATAKIWA FULHAM
KLABU ya Fulham inajaribu kumnunua kiungo wa Angers, Angelo Fulgini mwenye umri wa miaka 25, na wanaweza kufikia bei ya pauni milioni 18 kwa mchezaji huyo mzaliwa wa Ivory Coast. **(Sun)**

### GUARDIOLA ATETA NA BARCA
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekuwa na mazungumzo wakati wa chakula cha jioni na Mkurugenzi wa Soka wa Barcelona, Mateu Alemany na Mtendaji Mkuu, Ferran Reverter, huku mustakabali wa mshambuliaji Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21, ukiwa kati ya mambo yaliyojadiliwa. **(Mundo Deportivo)**

### TORRES KUBADILISHWA NA OLMA
KAMA Ferran Torres atakwenda Barcelona, Manchester City itafungua milango kwa kiungo wa kati wa RB Leipzig, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 23, kuhamia Etihad. **(El Nacional)**

### CITY KUSAJILI STRAIKA
MANCHESTER City wataangalia uwezekano wa kumsajili mfungaji mabao katika dirisha la usajili la Januari. **(Express)**

### PHILLIPS ATAKA GHAZI AUZWE
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Aston Villa, Kevin Phillips anaamini klabu yake ya zamani inapaswa kumuuza winga wa Uholanzi, Anwar El Ghazi mwenye umri wa miaka 26, katika dirisha la usajili la Januari. **(Football Insider)**

### PULISIC LULU LIVER, BARCA
LIVERPOOL na Barcelona zinamwania mshambuliaji wa Chelsea, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 23, lakini Blues hao hawawezi kumuuza mchezaji huyo kwa timu yoyote ya Ligi ya England, huku klabu hiyo ya Hispania ikiwa haina uwezo wa kutoa dau la euro milioni 50 linalohitajika ili kumsaini winga huyo wa Marekani. **(El Nacional)**

### SZALAI ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA imefanya mazungumzo na beki wa klabu ya Fenerbahce na Hungary, Attila Szalai mwenye umri wa miaka 23. **(Football Insider)**

### WOLVES KUMUUZA TRAORE
KLABU ya Wolves itasikiliza maombi ya kumuuza winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 25 katika dirisha la usajili la Januari. **(Football Insider)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CARRICK: SIJUI HATIMA YANGU MAN UNITED

**Kwa sasa, sijapata habari yoyote kuhusu hilo, hakika akili yangu ilikuwa kwenye mchezo dhidi ya Chelsea, kichwa changu...**

**LONDON, England**

MICHAEL Carrick aliiongoza Manchester United kupata pointi moja dhidi ya Chelsea wakati akisubiria kujua kama utakuwa mchezo wake wa kwanza na wa mwisho kwenye Ligi Kuu kuwa kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao.

Bao la ufunguzi la Jadon Sancho lilisawazishwa na Jorginho kwa mkwaju wa penalti pale Stamford Bridge, ambapo Carrick ambaye anaiongoza kwa muda timu hiyo, akimwanzisha benchi Cristiano Ronaldo juzi, Jumapili.

United ambayo ina mchezo wa nyumbani dhidi ya Arsenal Alhamisi hii, pengine unaweza kuwa wa kwanza chini ya Ralf Rangnick kama kocha wa muda.

Rangnick, kwa sasa anafanya kazi kule klabu ya Lokomotiv Moscow, na ndiye mtu ambaye Man United wamemteua kuwa kocha wa muda hadi mwishoni mwa msimu huu.

Kufukuzwa kwa Ole Gunnar Solskjaer Jumapili iliyopita baada ya kufungwa mechi tano mfululizo kati ya saba za Ligi Kuu, kulidhoofisha matumaini ya Man United kutoa changamoto ya kuwania taji la Ligi Kuu msimu huu.

Akizungumza baada ya sare ya bao 1-1 na Chelsea, Carrick aliwaambia waandishi wa habari kwamba, hajui nini kitaendelea kuhusu yeye.

"Kwa sasa, sijapata habari yoyote kuhusu hilo. Kwa hakika akili yangu ilikuwa kwenye mchezo huu. Kichwa changu kilikuwa kipo imara kwa ajili ya mchezo dhidi ya Chelsea tu," alisema. "Baada ya mchezo, nina uhakika nitakuwa najaribu kuzoea mazingira, na kuona nini kitatokea siku chache zijazo, lakini kwa sasa sijapata chochote cha kuwaambia."

MECHI KALI
HOME AWAY
MBEYA KWANZA FC
5.40 | 3.04 | 1.71
YOUNG AFRICANS

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 735

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GUARDIOLA: KIWANGO CITY HAKIJASHUKA MISIMU SITA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesema ni jambo la kujivunia kwamba, kiwango cha Manchester City hakijashuka kwa muda wa misimu sita mfululizo wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya West Ham juzi, Jumapili.

City waliifunga Everton mabao 3-0 Jumapili iliyopita kwenye Ligi Kuu kabla ya kuifunga Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano na siku nne baadaye wakawafumua West Ham.

Ilkay Gundogan alifunga bao la ufunguzi kwa wenyeji hao pale kwenye Uwanja wa Etihad ambao ulijaa barafu, huku Fernandinho aliyetokea benchi akifunga la pili na Manuel Lanzini akiwapa la kufutia machozi West Ham.

City, ambao sasa wamecheza mechi saba bila kuruhusu nyavu zao kutikiswa katika mechi nane zilizopita za Ligi Kuu nyumbani, imeshinda 10 kati ya 11 ilizokutana na West Ham.

Baada ya matokeo mengine ya kuridhisha, Guardiola alisifia kazi nzuri ya kikosi chake ambacho anaamini kushinda ndio sehemu ya mtindo wao wa uchezaji.

"Tulitengeneza nafasi nyingi dhidi yao, lakini la msingi ni kwamba tulipata pointi zote tatu," alisema Guardiola akiiambia BBC Sport.

"Dakika 15 hadi 20 za mwisho zilikuwa ngumu kucheza, lakini baada ya mchezo dhidi ya PSG tulijifunza kupambana kwa nguvu hadi dakika za mwisho, na hakika yalikuwa matokeo mazuri kwa upande wetu.

"Taji la Ligi Kuu England mara zote ndilo muhimu zaidi na ndio maana kila timu inacheza kwa kupambana kweli kweli.

"Baada ya kushinda mara tatu taji la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, ni rahisi tena kuwa kwenye nafasi ya kuliwania, kiwango chetu kimeendelea kuwa bora na hilo ni muhimu sana kwetu."

# Neymar aipa pigo PSG



**PARIS, Ufaransa**

MAURICIO Pochettino ana matumaini kwamba, Neymar hajaumia sana, ingawa picha za televisheni zilionyesha ana maumivu makali.

Neymar alitolewa nje kwa machela baada ya kuumia kifundo cha mguu wakati Paris Saint-Germain wakishinda dhidi ya Saint-Etienne Jumapili, muda mfupi baada ya Angel Di Maria kufanya matokeo kuwa 2-1 kwa vinara hao wa Ligue 1.

Halafu Marquinhos akafunga bao lake la pili kwenye mchezo huo na kufanya matokeo kuwa 3-1, na Pochettino alizungumzia hali ya Neymar baada ya mchezo huo.

Neymar alipigwa picha akionekana kuwa kwenye machela na Pochettino alielezea kuwa anasubiria kujua zaidi ameumia kwa kiasi gani.

"Sina cha kusema kwa wakati huu, ni maumivu ya mguu kwenye kifundo chake. Tutaona ameumia kwa kiasi gani," alisema Pochettino.

Pochettino baadaye aliiambia Amazon Prime: "Tunatakiwa kuangalia, lakini nina matumaini kwamba, atakuwa hajaumia sana. Lakini tukio lile halikuwa zuri sana."

## HABARI MICHEZO


# 5,865,580

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/12/21 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 02. 04/12/21 | 18:00 | Reading vs Hull City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 03. 04/12/21 | 18:00 | Bristol City vs Derby | 2.40 | 3.14 | 2.89 |
| 04. 04/12/21 | 18:00 | Barnsley vs Huddersfield | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 05. 04/12/21 | 18:00 | Newcastle vs Burnley | 2.24 | 3.31 | 3.21 |
| 06. 04/12/21 | 18:00 | Southampton vs Brighton | 2.42 | 3.30 | 2.90 |
| 07. 04/12/21 | 23:00 | Real Sociedad vs Real Madrid | 3.01 | 3.26 | 2.37 |
| 08. 05/12/21 | 14:30 | Bologna vs Fiorentina | 2.56 | 3.51 | 2.61 |
| 09. 05/12/21 | 16:00 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.30 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/12/21 | 17:00 | Lorient vs Nantes | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 11. 05/12/21 | 17:30 | QPR vs Stoke City | 2.36 | 3.23 | 2.89 |
| 12. 05/12/21 | 19:30 | Aston Villa vs Leicester | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 13. 05/12/21 | 20:30 | Levante vs Osasuna | 2.45 | 3.20 | 2.95 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**JUMANNE - 30 - NOVEMBA 2021**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:05 | 5504 | AL Draih vs AL Sahel SC | 2.75 | 3.05 | 2.75 |
| 15:20 | 3041 | Al Orubah vs AL Adalh | 2.94 | 3.09 | 2.29 |
| 15:30 | 4382 | Foolad Khuzestan vs Teraktor Sazi | 1.75 | 3.04 | 5.02 |
| 15:35 | 3338 | Ohud Medina vs Al Khaleej Club | 2.14 | 2.90 | 3.48 |
| 16:00 | 1448 | Mbeya Kwanza FC vs Young Africans | 5.40 | 3.04 | 1.71 |
| 16:00 | 1904 | Biashara United vs Polisi Tanzania | 2.46 | 2.51 | 3.38 |
| 16:00 | 5728 | Botev Plovdiv vs Botev Vratsa | 1.39 | 4.33 | 6.74 |
| 16:45 | 2291 | Bali Utd Pusam vs Persiraja Banda | 1.27 | 5.42 | 7.93 |
| 17:00 | 2342 | Delhi Dynamos FC vs East Bengal | 2.85 | 3.47 | 2.17 |
| 17:25 | 2625 | AL Nahdha vs AL Ain | 2.60 | 3.05 | 2.90 |
| 18:00 | 5295 | HNK Gorica vs Istra | 1.64 | 3.62 | 4.64 |
| 18:30 | 3124 | Beroe vs Slavia Sofia | 1.83 | 3.32 | 3.95 |
| 19:00 | 5102 | Azam vs Mtibwa Sugar | 1.48 | 3.56 | 6.93 |
| 19:30 | 3628 | Qatar vs Bahrain | 1.41 | 3.87 | 7.54 |
| 20:00 | 1954 | Cremonese vs Frosinone | 2.40 | 3.09 | 2.94 |
| 20:00 | 2421 | Pisa vs Perugia | 2.29 | 3.08 | 3.13 |
| 20:00 | 4598 | Korona Kielce vs Gornik Leczna | 2.37 | 3.12 | 2.79 |
| 20:00 | 5173 | Maccabi Petach Tikva vs Hapoel Hadera | 2.35 | 3.04 | 2.89 |
| 20:30 | 1037 | Lokomotiva Zagreb vs Hajduk Split | 3.71 | 3.38 | 1.87 |
| 20:30 | 3400 | Maccabi Netanya vs FC Ashdod | 2.04 | 3.38 | 3.19 |
| 20:30 | 4313 | Atalanta vs Venezia | 1.26 | 6.00 | 10.00 |
| 20:30 | 5785 | Fiorentina vs Sampdoria | 1.63 | 4.11 | 4.91 |
| 21:15 | 5763 | Bnei Sakhnin vs Beitar Jerusalem | 2.35 | 3.17 | 2.79 |
| 21:30 | 3826 | Chindia Targoviste vs Sepsi Osk | 2.70 | 2.89 | 2.60 |
| 22:30 | 1220 | Reggina vs Ascoli | 2.19 | 3.19 | 3.24 |
| 22:30 | 2159 | Vicenza vs Benevento | 3.34 | 3.19 | 2.14 |
| 22:30 | 3299 | Monza vs Cosenza | 1.62 | 3.64 | 5.31 |
| 22:30 | 4487 | Pordenone vs Alessandria | 2.46 | 3.05 | 2.90 |
| 22:30 | 5279 | Spal vs Lecce | 2.93 | 3.08 | 2.41 |
| 22:30 | 5550 | Newcastle vs Norwich City | 1.94 | 3.60 | 3.75 |
| 22:45 | 1045 | Warrenpoint vs Ballymena Utd | 3.27 | 3.71 | 1.91 |
| 22:45 | 1053 | Linfield Belfast vs Carrick Rangers | 1.21 | 5.99 | 9.47 |
| 22:45 | 1283 | Tranmere vs Harrogate | 2.12 | 3.47 | 2.94 |
| 22:45 | 1495 | CD San Jose vs Oriente Petrolero | 8.27 | 5.39 | 1.26 |
| 22:45 | 1509 | Motherwell vs Dundee Utd | 2.33 | 3.15 | 3.05 |
| 22:45 | 1809 | Accrington vs Wigan | 2.99 | 3.47 | 2.09 |
| 22:45 | 2289 | Farsley Celtic vs Stalybridge | 1.84 | 3.62 | 3.57 |
| 22:45 | 2947 | RFC Seraing vs Anderlecht | 4.80 | 3.92 | 1.61 |
| 22:45 | 3251 | Verona vs Cagliari | 1.60 | 4.21 | 5.01 |
| 22:45 | 3717 | Cove Rangers vs Glasgow Rangers FC B | 1.52 | 4.60 | 5.40 |
| 22:45 | 4079 | Wrexham vs Yeovil | 1.62 | 3.86 | 4.79 |
| 22:45 | 4177 | Salernitana vs Juventus | 7.23 | 4.63 | 1.42 |
| 22:45 | 5010 | Exeter vs Bradford City | 2.26 | 3.40 | 2.96 |
| 22:45 | 5158 | Inverness vs Raith Rovers | 2.01 | 3.47 | 3.18 |
| 22:45 | 5203 | Dungannon Swifts vs Glenavon | 3.66 | 3.95 | 1.74 |
| 22:45 | 5747 | Larne vs Cliftonville Belfast | 1.80 | 3.61 | 3.75 |
| 22:45 | 5985 | Coleraine FC vs Glentoran Belfast | 2.33 | 3.51 | 2.60 |
| 22:45 | 5999 | Ashton Utd vs Guiseley | 3.04 | 3.57 | 2.04 |
| 23:15 | 2108 | Leeds vs Crystal Palace | 2.43 | 3.30 | 2.90 |
| 23:15 | 3416 | Sporting Braga vs FC Vizela | 1.38 | 4.74 | 7.11 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MTIBWA YAKATA UZITO WA KIFARU



**Na Dennis Fussi**

MATOKEO yasiyoridhisha ya timu ya Mtibwa Sugar yamesababisha Ofisa Habari wake, Thobias Kifaru kudai anapungua kilo moja kwenye uzito wake kila siku, kwa sababu ya mawazo kutokana na kiwango kibovu cha timu hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Azam FC utakaopigwa leo kwenye Uwanja wa Chamazi, Dar es Salaam, Kifaru amesema yeye pamoja na uongozi wa klabu ya Mtibwa hawaridhishwi kabisa na kiwango pamoja na matokeo ya timu hiyo.

Alisema kama uongozi wamekuwa wakifanya kila kitu kinachowezekana kuhakikisha Mtibwa ambayo ilikuwa kiboko ya vigogo hapo awali inarudi kwenye kiwango chake, huku sasa ikiwa inaburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu kwa kupata pointi mbili pekee.

Akizungumza kwa uchungu, Kifaru alisema uongozi wa Mtibwa umekuwa ukifanya jitihada za makusudi na kila mara kukaa vikao na wachezaji wao na kuzungumza nao kuhusu matokeo hayo mabaya.

"Kiukweli napungua uzito wa kilo moja kila siku kutokana na mawazo ya matokeo mabovu ya timu yetu ya Mtibwa, kwani tumekuwa tukifanya kila kitu kwa wachezaji, lakini mambo ni tofauti kabisa," alielezea Kifaru.

Aliongeza: "Wachezaji wote wamekuwa wakilipwa mishahara yao kwa wakati kabla ya mwezi unaofuata, wanalala sehemu nzuri sana, wanakula chakula bora kabisa, lakini uongozi unashindwa kuelewa tatizo liko wapi."

Kifaru alisema baada ya matokeo hayo mabaya, sasa wamejipanga kuhakikisha kwamba, mchezo wao dhidi ya Azam wanapata matokeo chanya na kuhakikisha wanaibuka na ushindi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi kwenye ligi hiyo.

"Bado tuna matumaini makubwa na timu yetu, kwamba, pengine tumeanza vibaya, lakini tutamaliza vizuri, ingawa mwenendo wa timu umeuweka uongozi kwenye wakati mgumu sana.

"Sasa mechi yetu dhidi ya Azam tutapambana na kikubwa tunataka kuhakikisha tunaibuka na ushindi," alisema Kifaru.

Mtibwa ambayo kwa sasa inanolewa na kocha Joseph Omog kutoka nchini Cameroon, imeshawahi kushinda mara mbili ubingwa wa Ligi Kuu katika historia yake na pia imekuwa moja ya timu iliyotoa wachezaji wengi zaidi waliotamba na wanaotamba kwenye klabu kubwa kama Simba, Yanga na Azam.

Kwa sasa Mtibwa inashika mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi mbili baada ya kushuka dimbani mara sita ikitoka sare mbili na imepoteza mechi nne.

# Omog amwekea rada Tambwe



**Na Dennis Fussi**

KLABU ya Mtibwa Sugar ina mpango wa kuibomoa timu ya DTB kwa kumsajili mshambuliaji wake namba moja Amissi Tambwe kwenye dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, amesema uongozi wa timu hiyo tayari umeanza mazungumzo na wenzao wa DTB ili kukamilisha dili hilo mapema.

"Ni kweli kocha wetu Joseph Omog amevutiwa na Tambwe na ameuagiza uongozi kulishughulikia suala hilo ili mzunguko wa pili ukianza tuwe naye," alisema Kifaru.

Tambwe amedhihirisha ubora wake katika ufungaji baada ya kufunga mabao tisa kwenye ligi ya Championship na amewahi kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu nchini akiwa na Simba na Yanga.

Michezo
Jumanne Novemba 30, 2021
Nipashe



Carrick: Sijui hatima yangu Man United

UKURASA 21

# MORRISON AOMBA RADHI SIMBA, PABLO AWAONYA

## ●●●Aimulika Geita Gold huku akitaka kuepuka ya Jwaneng Galaxy...

**Na Saada Akida**

SHUJAA wa mechi ya juzi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Simba na Red Arrows ya Zambia, Bernard Morrison, amewaangukia mashabiki, viongozi na washikadau wote wa klabu hiyo huku akiahidi furaha kubwa zaidi, lakini Kocha Mkuu wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Pablo Franco, ametoa onyo kali kwa wachezaji wake.

Simba juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ilitanguliza mguu mmoja ndani kufuzu hatua ya makundi baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Wazambia hao, huku Morrison akihusika katika mabao yote matatu baada ya kufunga mawili na kutengeneza moja.

Akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, ambayo alionyesha kiwango cha hali ya juu, Morrison alisema walitaka kuutumia mchezo huo kwa kuomba msamaha kupitia matokeo chanya, kutokana na kufanya vibaya kwenye mechi iliyopita ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

"Napenda kusema samahani kwa mashabiki, uongozi wa Simba na washikadau wote wa Simba, kwa kutofanya vizuri katika mechi ya hivi karibuni, tulitaka kutumia huu mchezo kuomba msamaha kwao wiki ijayo [wiki hii] tutafuzu na kurejesha furaha kubwa tena," alisema Morrison.

Hata hivyo, wakati Morrison akishuka maneno hayo ya faraja kwa Wanasimba, Kocha Mkuu, Pablo amewaonya wachezaji wake, akiwataka kusahau matokeo hayo na kuelekeza akili zao katika mechi ya Ligi Kuu kesho dhidi ya Geita Gold FC na baada ya hapo mchezo wa marudiano dhidi ya Red Arrows kwa kuwa hizo ni dakika 90 tu za mwanzo bado hawajamaliza kazi.

Simba kesho itaikaribisha Geita Gold katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kwenda Zambia kurudiana na Red Arrows Jumapili wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Pablo alisema furaha yake si kubwa sana kwa sababu wamemaliza dakika 90 za mwanzo na hawajamaliza mchezo huo kwa kuwa bado wa dakika 90 za kipindi cha pili ambazo ni muhimu zaidi kwao.

Alisema mechi ya marudiano itakuwa ngumu kwa sababu wapinzani wao, Red Arrows, watacheza uwanja waliouzoe na ameshuhudia timu nyingi zinavyobadilisha matokeo, hivyo huu ni wakati wa kujipanga zaidi ili hilo lisijitokeze katika mechi ya marudiano.

"Kwa hali ilivyokuwa, namna timu ilivyoimarika na namna kila mmoja anavyopambana, nimefurahi lakini si sana kwa sababu bado tuna mchezo wa ugenini ambao tutakutana na timu ngumu.

"Nimeshuhudia timu nyingi zinavyoweza kubadilisha matokeo, wachezaji wanatakiwa kuwa makini na kutojisahau kwa ushindi huu, ukiangalia Red Arrows wako vizuri kuliko Jwaneng Galaxy ambayo ilituondoa katika Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Pablo.

Alisema atatumia mechi yao ya ligi dhidi ya Geita Gold FC kutafuta matokeo ya ushindi, lakini kufanyia kazi mapungufu yao kuelekea kujiandaa vizuri kwa mchezo wao wa marudiano ambao ni muhimu kupata ushindi.



Morrison

# Yanga bila Bangala kwa Mbeya Kwanza

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, leo wataingia kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kucheza dhidi ya Mbeya Kwanza iliyopanda daraja msimu huu, ikiwa ni mechi ya raundi ya saba.

Yanga, yenye pointi 16 itaingia uwanjani ikisaka ushindi ili iweze kujichimbia kwenye kilele cha msimamo wa ligi, na kama ikipata ushindi, itafikisha pointi 19. Hata hivyo, itaingia ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo Novemba 20, mwaka huu, na kutibua rekodi yake ya ushindi wa asilimia 100, baada ya kushinda mechi tano mfululizo.

Kocha msaizidi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wanajua umuhimu wa mechi hiyo na pointi zake na hii ni baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC.

"Baada ya mechi ile tumekaa benchi la ufundi na wachezaji, tumefanya tathmini na kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza. Najua tatizo linaweza kuwa uwanja kwa sababu vingi vya mikoani si rafiki, lakini kama tunataka ubingwa tunapaswa tujipange kucheza kwenye kila mazingira. Tumejiandaa vizuri, ila tutamkosa Yannick Bangala kwa sababu ana kadi tatu za njano," alisema kocha huyo.

Wenyeji Mbeya Kwanza mpaka sasa wanakamata nafasi ya 11, wakiwa wamecheza mechi sita, wakishinda moja, sare nne na kupoteza moja.

Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza, Haruna Hererimana, amesema hatobadili mfumo wake wa uchezaji eti kwa sababu anacheza na Yanga, badala yake atacheza vile vile kikubwa ni umakini tu kwa wachezaji wake ndiyo unaohitajika.

"Mimi sibadilishi mfumo, si kwa sababu tunacheza na Yanga ndiyo tuanze kubabaika, tutapambana tu kwa sababu hata wachezaji wangu ni wazuri, kikubwa kinachohitajika ni umakini tu," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >